# Nipashe

Jumatatu Julai 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581017

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 295,393,790

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**RIPOTI MAALUM:** Miti inapokatwa kupisha mabango

UKURASA 4




UKURASA 22

## HATIMA YA NEYMAR PSG HAIJULIKANI



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza kwa simu na waendesha bodaboda jijini Dodoma jana. **PICHA: MAKTABA**

# Nasaha za Samia kwa waendesha bodaboda, bajaj

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### MJADALA MKATABA WA TICTS WASHIKA KASI MTANDAONI

MJADALA wa Kampuni ya Kimataifa ya Kuhudumia Makontena (TICTS) kuhusu kuongezewe mkataba au la jana ulishika kasi kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine ...

UKURASA WA 3

### MCHUNGAJI ADAIWA KUFARIKI AKIONGOZA IBADA YA MAZIKO

MCHUNGAJI wa Free Pentecost Church of Tanzania (FPCT), Kata ya Ndanda, wilayani Masasi mkoani Mtwara, Laurence Milanzi, anadaiwa kufariki dunia wakati akiendesha...




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini akiangalia msaada wa madawati kati ya 400 yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya shule tano za Jiji la Mbeya, huku wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari Iduda wakiketi katika madawati hayo. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHADEMA yakosoa Sheria ya Wanyamapori

UKURASA 3

NYONGEZA MSHAHARA

# Serikali, TUCTA kukutana kesho

UKURASA 2


MICHEZO | MAYELE MIAKA MIWILI YANGA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Nasaha za Samia kwa waendesha bodaboda, bajaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewausia waendesha bodaboda na bajaji nchini kuacha tabia ya kujihusisha na matukio ya ujambazi na uporaji wa mali za raia kwa kutumia vyombo vyao vya usafirishaji.

Mkuu huyo wa nchi alitoa wosia huo jana alipopiga simu na kuzungumza na madereva wa vyombo hivyo katika kongamano la kuimarisha ushiriki wa kundi hilo katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na matukio ya waendesha bodaboda na bajaji kuhusika katika matukio ya uhalifu ikiwamo uporaji wa mali pamoja na ujambazi.

"Nawaombeni msiwe sehemu ya matukio ya uhalifu nyinyi ni kundi muhimu sana katika nchi yetu huduma yenu ya usafiri mnahudumia kundi la watu wa chini hivyo kujihusisha na matukio ya kihalifu sio jambo jema nawaombeni muache mara moja vitendo hivi.

"Najua kati yenu wapo wasomi nawaombeni msikubali baadhi yenu wenye tabia hizo wawachafulie jina lenu, mimi nipo pamoja na nyie changamoto zenu zinazoawakabili nazisubiri ziletwe kwangu ili tuzifanyie kazi mara moja," alisisitiza.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, ambaye ndiye mratibu wa kongamano hilo kusikiliza changamoto za kundi hilo na kuzifikisha kwake ili azifanyie kazi.

Aidha, aliwataka bodaboda na bajaji nchini kushiriki katika tukio la kitaifa la sensa ya watu na makazi ambalo limepangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Nawaombeni mwende kuwa mabalozi wakubwa katika jambo hilo ili kufanikisha kufanyika kwa ufanisi na kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi na kupanga mipango yake ya maendeleo," alisisitiza Rais Samia.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alisema wamekutana na kundi hilo kutokana na kuwahudumia wanachi wengi na kwamba itakuwa rahisi kuwafikia watu wengi na kuwahamasisha kushiriki sensa ya watu na makazi.

"Ndugu zangu nyie wa bodaboda na bajaji serikali yetu imetumia kiasi kikubwa sana cha fedha kufanikisha zoezi hili la sensa ya watu na makazi kwani hapa kwetu wakufunzi zaidi ya 400 wanafundishwa ili kwenda kuwafundisha makarani zaidi ya 10,000, hivyo haitakuwa jambo la busara kama hamtashiriki kuhamasisha watu kujitokeza ili serikali ipate takwimu zitakazo saidia kwenda kupanga mipango ya maendeleo," alisema.

Kamisaa wa sensa ya watu na makazi Zanzibar, Balozi Mohamed Ali Hamza, alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kuwa mstari wa mbele kukutana na makundi mbalimbali katika kuhamasisha kutushiriki katika sensa ya watu na makazi.


"Mkuu wa mkoa wa Dodoma tunakushukuru sana kwa kuendelea kutushirikisha katika matukio yanayohusu jambo hili la kitaifa la sensa ya watu na makazi na tunatumaini kundi hili litatusaidia sana kwenda kufikisha ujumbe huu ili sensa ya mwaka huu iwe na ufanisi mkubwa sana," alisema.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema sensa ni takwa la kisheria sio hiyari na inamataka kila mwananchi kutoa takwimu sahihi ambazo zitaisaidia serikali kupanga mipango yake bila kumwacha mtu nyuma.

"Hii ni sensa ya sita toka mwaka 1964 na inakwenda kufanyika kidijitali zaidi, tunamshukuru sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza fedha nyingi ili kufanya sensa hii kuwa na ufanisi mkubwa," alisema.

Mkuu wa mkoa wa Dodoma aliwataka waendesha bodaboda na bajaji nchini kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia sheria za nchi na kuacha kujichukulia hatua mkononi.

"Bodaboda na bajaji ni kazi ya heshima sana hampaswi nyinyi kufanya mambo ya ovyo leo hii dereva wa bodaboda akikwanguliwa tu na gari wote wanaizonga gari ile na kutaka kujichukulia hatua mkononi msifanye hivyo kwani mtakua chakula cha sheria na chakula cha sheria kinaanzia katika kituo cha polisi na hatimaye mahakamani," alisema Mtaka.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman, Mohammed Nasser Al Wahaibi (wa pili kulia) na ujumbe wake walipofika Ikulu Zanzibar akiongozana na Balozi wa Oman nchini Tanzania, Saud Hilal Al Shidhani na Balozi mdogo wa Oman anayefanyia kazi zake Zanzibar, Said Salim Al Sinawi. **PICHA: IKULU**

## Mjadala mkataba wa TICTS washika kasi

**Na Mwandishi Wetu**

MJADALA wa Kampuni ya Kimataifa ya Kuhudumia Makontena (TICTS) kuhusu kuongezewe mkataba au la jana ulishika kasi kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine wakiishauri serikali kufungua zabuni ya kimataifa kupata wengine.

Hatua hiyo imekuja kutokana na mkataba wa kampuni hiyo kukaribia kumalizika wiki ijayo.

Katika ukurasa wake wa twitter Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika "Si mkataba unakwisha? Kama ndiyo Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), itangaze zabuni yenye ushindani ya kimataifa, kama wakishinda (TICTS) poa waendelee. Lazima Tanzania inufaike na Jiografia yake, haiwezi kuendelea hivi."

Kwenye mitandao hiyo kulikuwa na upigaji kura kwa wanaotaka kampuni hiyo iendelee au itangazwe zabuni, huku wengine wakisema utendaji haukuwa wa kuridhisha wakitaka TPA ifanye kazi hiyo yenyewe.

"Kwanini tusichunguze, kwanini walishindwa kufanyakazi kwa ufanisi kabla ya kuwachukulia hatua, ni lazima kuangalia vikwazo dhidi yao katika utoaji huduma, labda mazingira hayakuwa rafiki," aliandika mmoja wa wananchi na kuongeza:

"Mimi ni mteja wa bandari, ni dereva wa magari ya mizigo hawa watu hawako makini kwasababu hatupati huduma kwa wakati."

Mchangiaji mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Joe, alisema "nakumbuka nilifanyakazi kwenye kampuni fulani Mwanza kuanzia mwaka 2016-2018, bosi wangu alikuwa anatumia Bandari ya Mombasa nchini Kenya kupitisha makontena yake kutokana na urasimu uliokuwapo katika bandari ya Dar es Salaam, ni muhimu mamlaka zikafuatilia na kufanyia mabadiliko."

Naye Ali Mohamed, mkazi wa Dar es Salaam, alisema "TICTS wanafanyakazi nzuri pale, mimi ni wakala nawafahamu kwa miaka mingi, wanatuhudumia vizuri na bila wao huenda bandari yetu ingeshakufa, wana vifaa vya kisasa nadhani kuna siasa katika hili."

Aidha, wachangiaji hao walitaka serikali kutafuta mwekezaji mwingine kama haitatoa mkataba mwingine, huku wakitaka kuwekwa vipengele vya kuwabana kuondoa kasoro zilizojitokeza.

Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano uliosainiwa mwaka 2017 kati ya TICTS na TPA, unatakiwa kuhuisha mkataba wa miaka mitano mwezi Agosti/Septemba mwaka huu kwa kadiri watakavyoridhika na utendaji kazi wao.

NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**M/HAKIMU MKAZI MWANZA - SHAURI LA MADAI NA. 5/2022**
**JOHN KIMORI ______________MDAI**
**DHIDI YA**
**ADAM BALENGA ______________MDAIWA**

**M/MWANZO ILEMELA – SHAURI LA MADAI NA. 127/2021**
**BIBIANA BUGINGO _________________MDAI**
**DHIDI YA**
**FREDRIKA SELESTINE_________________MDAIWA**

**M/MWANZO BUKUMBI - SHAURI LA TALAKA NA. 10/2020**
**DIANA IBRAHIM _______________MDAI**
**DHIDI YA**
**SIMON JOHN__________________MDAIWA**

216958502

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA, MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA NA MAHAKAMA YA MWANZO BUKUMBI, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA NA KIWANJA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA NA.10 KITALU "P" ILIYOPO MTAA WA RUFIJI | MTAA WA RUFIJI - MWANZA | 25/08/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | KITONGOJI CHA MTAKUJA KATA YA USAGARA, WILAYA YA MISUNGWI MKOA WA MWANZA. | 26/08/2022 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | KIWANJA NA. 936 KITALU "G" KILICHOPO NYASAKA | NYASAKA - MWANZA. | 25/08/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI ISIYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

## Serikali, TUCTA kujadili nyongeza mishahara kesho

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema inatarajia kukutana na viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) kesho, ili kusikiliza malalamiko ya watumishi kuhusu nyongeza ya mshahara kwa asilimia 23.3 na kutoa ufafanuzi.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa katika ukurasa wa kijamii wa Twitter ilisema:

"Ndugu wafanyakazi, Jumanne tarehe 26 Julai, 2022, serikali itakuwa na viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi ili kuwasikiliza na kutoa ufafanuzi kuhusu nyongeza ya mishahara katika mishahara ya Julai, 2022."

Kabla ya taarifa hiyo, juzi aliandika Twitter kuwataka watumishi hao kuwa watulivu wakati serikali ikitoa ufafanuzi.

Msemaji huyo na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya kuwepo mjadala kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kiwango cha fedha kilichoongezwa.

Alfonce Daniel, mtumishi mkoani Singida, alisema ongezeko hilo limemshtua kwa sababu ni tofauti na alichokitarajia kutokana na kiwango cha mshahara wake.

"Nimeshtuka sana kwa sababu asilimia 23.3 ya mshahara wangu sio Sh. 60,000. Mara ya kwanza nikahisi kuwa labda nitaongezwa, lakini siku zinazidi kwenda sioni kitu. Kuna haja ya serikari kutupa ufafanuzi unaoeleweka kuhusu suala hili," alisema.

Naye Anastazia James (sio jina lake halisi), alisema licha ya serikali kutoa ufafanuzi wa nyongeza ya mishahara bado inampa ugumu kuelewa kwa sababu anaona kuwa inakinzana na asilimia 23.3 iliyotangazwa na serikali.

"Mshahara wangu ni Sh. 710,000 lakini nyongeza nimepata Sh. 65,000 ambayo ni asilimia 7.7. Naona kama hakuna uwiano kwanini mimi nipate hiyo halafu mwingine apate asilimia 23.3 tofauti na kauli ya serikali, hapa kwa kweli nahitaji kupata ufafanuzi unaoeleweka," alilalamika Anastazia.

Alipotafutwa na Nipashe, Katibu Mkuu wa TUCTA, Henry Mkunda, alisema kuwa wanasubiri kikao kati yao na serikali pamoja na waraka wa serikali ndipo watatoa tamko.

"Tutaongea tukiwa na kitu mkononi, ndiyo maana hata baada ya kutangaziwa ile asilimia 23 tulikuwa tunasubiri waraka na mishahara itoke huu mwezi wa saba, ili watu waone exactly (hasa) ni nini halafu baada ya hapo tunakuwa na nafasi nzuri ya kuzungumza vizuri, kama Jumanne tunakutana na serikali kuzungumza naamini mambo yatakuwa sawa tu," alisema Henry.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai (wa pili kulia) pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule (katikati), wakipokea bendera kwa mmoja wa washiriki wa kampeni ya GGM Kili Challenge waliopanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kuchangia fedha za kuendeleza mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda na nyuma yao aliyevaa kofia ni Makamu Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simona Shayo. Hafla ya mapokezi hayo ilifanyika mwishoni mwa wiki katika lango la Mweka Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.** **HABARI UK. 5**

# CHADEMA yataka Sheria ya Wanyamapori kufumuliwa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimependekeza kufumuliwa kwa Sheria ya Wanyamapori namba tano ya mwaka 2009, ili kuwalinda wananchi ambao wanakumbwa na madhira ya kuharibiwa mali, kujeruhiwa na kuuawa na wanyama.

Chama hicho pia kimeitaka serikali kuweka ulinzi dhidi ya uvamizi wa wanyamapori kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na maeneo yaliyohifadhiwa nchini.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wa chama hicho, Julius Mwita, kwa sasa sheria hiyo inatoa kipaumbele zaidi kwa wanyama kuliko kwa binadamu.

"Ni muhimu tukaikumbusha serikali na mamlaka zinazohusika kwamba, sehemu kubwa ya hifadhi za taifa zimepakana na maeneo ya makazi ya wananchi, hivyo kusababisha migogoro ya mara kwa mara baina ya wanyamapori na wananchi wanaoishi maeneo hayo, lakini waathirika wakuu ni wananchi kwa kuwa sheria zilizoko kwa sasa haziwalindi wala kuwathamini wananchi," alibainisha Mwita.

"Kifungu cha 71(1), (2) na (3) kinahusika na kifuta machozi kwa mtu au kundi la watu ambao wameumizwa au kupoteza maisha, mifugo, mazao au kusababishiwa majeraha na wanyama wakali. Kifungu hiki hakiongelei fidia kwa athari zinazosababishwa na wanyamapori," alisema na kuongeza:

"Na waziri amepewa mamlaka ya kutunga kanuni zinazosimamia ulipwaji wa kifuta machozi hicho na kuwekewa tahadhari kuwa kama ni mazao, kifuta machozi hicho kisizidi ekari tano. Mapungufu haya ya sheria yanawanyima haki wananchi ambao mazao yao yanaharibiwa na wanyama hata pengine mifugo au watu kudhuriwa na wanyama hatari."

"Ukisoma vifungu husika utaona sheria inatetea haki za wanyama kuliko za binadamu hata pale wanyama wakiingilia makazi ya watu. Aidha, sheria haisemi fidia bali kifuta jasho. Kifungu hiki kinacheza na maisha ya wananchi wetu na kuendelea kuwapa wanyamapori thamani kubwa kuliko binadamu."

Alisema ni vyema sheria ikafanyiwa marekebisho na ikaeleza kwamba wananchi walipwe fidia kulingana na uhalisia wa uharibifu wa mazao yao.

"Bunge la wananchi tunapendekeza sheria iwezeshe mamlaka za hifadhi kuanzisha mfuko maalum wa fidia kwa wananchi, sehemu ya mapato ya hifadhi iwekwe moja kwa moja kwenye mfuko huu wa fidia. Serikali iweke mipaka ya waya za umeme baina ya hifadhi na vijiji vya jirani ili kuzuia wanyama kuvuka na kushambulia vijiji na mazao yao," alisema Mwita.

Alipendekeza serikali iweke utaratibu wa idadi ya wanyama kwenye baadhi ya mbuga kwa kuwahamishia kwenye wanyama wachache ili wapate malisho na kushiba.

"Hiyo itawafanya wanyama wabakie ndani ya hifadhi husika kwani watapata malisho ya kutosha na hili litafanyika kwa ufanisi endapo Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) itatoa takwimu kwa uwiano wa hifadhi zenye wanyama wengi na zenye wachache," alisema Mwita. Pia, alipendekeza serikali kuanza kuweka utaratibu wa kuwa na vitalu maalum ndani ya maeneo ya uhifadhi kwa ajili ya kukabiliana na msimu kiangazi.

"Vitalu hivi viwekwe maalum kwa ajili ya malisho na maji wakati wa misimu ya kiangazi, yachimbwe mabwawa ndani ya mbuga na nyasi zimwagiliwe nyakati za ukame. Maeneo haya yafunguliwe wakati wa msimu wa kiangazi ili kutoruhusu wanyama kutoka nje ya maeneo yao," alisema. "Wananchi waelimishwe namna ya kutambua ushoroba wa wanyama hasa tembo pamoja na kutambua uwanda, ili waepuke kulima kwenye maeneo hayo na usumbufu wa wanyama ambao wananchi wanakuwa wamewafuata wanyama kwenye njia zao. Haki za binadamu ipewe kipaumbele kwa mujibu wa sheria ya wanyamapori, mchango wa mashirika kwa jamii iwe ni lazima kwa vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi za taifa au mapori ya akiba na wananchi wahusishwe katika uhifadhi kwa kuweka mwakilishi wa wananchi katika bodi za hifadhi za Taifa."

Katika Bunge la Bajeti, wabunge waliuliza maswali ya msingi na nyongeza kuhusu kukithiri kwa madhara upande wa binadamu wanaoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa, huku wakiomba serikali kuja na mkakati wa kuwanusuru huku wakitaka wavunwe.

Akijibu maswali ya papo kwa papo kila Alhamisi bungeni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali haikusudii kuwavuna bali inafanya tathmini ya uharibifu ili kuchukua hatua huku kukiwa na mpango wa kujenga vituo 32 vya kufukuza wanyama.

Wiki iliyopita, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, akitoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti tangu Julai mosi, mwaka huu, alisema serikali itajenga vituo 19 vya kambi za askari kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema lengo ni kukabiliana na uharibifu mazao ya wananchi unaofanywa na wanyamapori wakali, ikiwa ni hatua ambayo imetokana na kuwapo kwa matukio mengi ya wanyamapori hao kufanya uharibifu wa mazao ya wananchi.

# Mchungaji adaiwa kufariki akiongoza ibada ya maziko

**Na Said Hamdani,** MASASI

MCHUNGAJI wa Free Pentecost Church of Tanzania (FPCT), Kata ya Ndanda, wilayani Masasi mkoani Mtwara, Laurence Milanzi, anadaiwa kufariki dunia wakati akiendesha ibada ya kuombea mwili kabla ya kuingizwa kaburini.

Tukio hilo lilitokea wakati wa maziko hayo Julai 20, mwaka huu, katika makaburi ya Kijiji cha Liputu.

Imedaiwa kuwa marehemu Daudi Veno, ambaye alikuwa muumini wa Kanisa Katoliki, hakuwa anahudhuria ibada kanisani kwake hatua iliyosababisha viongozi wa kanisa hilo kutoshiriki maziko hayo, ndipo mchungaji huyo alipokubali kumzika.

Imeelezwa kuwa wakati wakiwa makaburini mchungaji huyo akiongoza ibada alijitokeza mwanamke mmoja ambaye jina lake halikufahamika mara moja na kuhoji uamuzi wa mchungaji huyo.

Chanzo cha habari kimeeleza kuwa Mchungaji Milanzi alijibu kuwa kutoongoza ibada ya maziko ni kuihukumu maiti na kwamba jukumu hilo ni la Mungu.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema walipofika makaburini wakati ibada ikiendelea na kufikia wakati wa kuingizwa kaburini, Mchungaji Milanzi alisema anachukua jukumu hilo kutokana na imani na kitabu kinavyomwongoza.

"Nachukua jukumu hili kuwaomba viongozi wenzangu, huyu aliyefariki ni mfuasi wenu suala la kutohudhuria kanisani mwachieni Mungu atoe hukumu yake," alinukuliwa na shuhuda wa maziko hayo.

Mashuhuda hao walidai baada ya kutoa nasaha kwa watu kutosusia kumzika mtu, ghafla alidondoka chini, lakini alipopelekwa Hospitali ya Mission ya Ndanda, ilibainika ameshafariki dunia.

Mmoja wa madaktari wa Hospitali ya Ndanda ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa sio msemaji, alithibitisha kupokelewa mwili wa Mchungaji Milanzi na kuhifadhiwa chumba cha maiti.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicodemus Katembo, alipotafutwa kupitia simu ya mkononi alithibitisha kupata taarifa za kifo cha mchungaji huyo na kwamba ni cha kawaida kama vifo vingine.

"Taarifa hiyo ya kifo cha Mchungaji Milanzi ninayo kweli, ni kifo cha kawaida kama vingine tu," alisema Katembo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA**
**SHAURI LA MAREJEO NA. 1 OF 2022**
**(Linatokana na shauri asilia la madai No.03/2018 Mahakama ya Mwanzo Ilemela na maombi madogo Na.5/2022 kutoka Mahakama ya Wilaya Ilemela.)**
**NGONZI SEFOLOZA BYAMUNGU......MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ROMULUZI EMMANUEL MSUNGA...MJIBU MAOMBI**
**KWA; ROMULUZI EMMENUEL MSUNGA**
**S.L.P**
**MWANZA.**

**AU POPOTE WALIPO TANZANIA,**

**KUITWA SHAURI**

Kwa kuwa mdai ameleta rufaa katika mahakama hii na Rufaa hiyo imepangwa kutajwa mbele ya Mheshimiwa P.P KUBAJA, Hakimu mfawidhi tarehe 28 mwezi July 2022 saa 10:00 Asubuhi.
Hivyo mnatakiwa kuhudhuria bila kukosa au mwakilishi wenu ili kusikiliza rufaa.
Hati hii imetolea kwa amri yangu na muhuri wa Mahaka hii leo tarehe 14 mwezi July, 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA ILEMELA

**KUPOTELEWA NA LESENI ZA MACHIMBO**

**NDG.ZUENA ABDU ALI**
Anatangaza kupotelewa na leseni za machimbo kama ifuatavyo :

PML 000343 SWZ (MBE/MBE/RB/291260/2022),PML 000344 SWZ (MBE/MBE/RB/291279/2022),
PML 000344 SWZ (MBE/MBE/RB/291279/2022),PML 000345 SWZ (MBE/MBE/RB/291283/2022),
PML 000346 SWZ (MBE/MBE/RB/291286/2022),PML 000347 SWZ (MBE/MBE/RB/291294/2022),
PML 000348 SWZ (MBE/MBE/RB/291288/2022),PML 000349 SWZ (MBE/MBE/RB/291290/2022),
PML 000350 SWZ (MBE/MBE/RB/291291/2022),PML 000351 SWZ (MBE/MBE/RB/291293/2022).

Kwa yeyote atakayeziona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi kilicho karibu.Taarifa za polisi zipo kwenye mabano.

**KUPOTELEWA NA LESENI ZA MACHIMBO**

**ZUENA ABDU ALI**
Anatangaza kupotelewa na leseni za machimbo kama ifuatavyo:

PML 000334 SWZ (MBE/MBE/RB/291251/2022),PML 000335 SWZ (MBE/MBE/RB/291261/2022),
PML 000336 SWZ (MBE/MBE/RB/291265/2022),PML 000337 SWZ (MBE/MBE/RB/291270/2022),
PML 000338 SWZ (MBE/MBE/RB/291275/2022),PML 000339 SWZ (MBE/MBE/RB/291276/2022),
PML 000340 SWZ (MBE/MBE/RB/291277/2022),PML 000341 SWZ (MBE/MBE/RB/291254/2022),
PML 000342 SWZ (MBE/MBE/RB/291257/2022).

Kwa yeyote atakayeziona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi kilicho karibu.Taarifa za polisi zipo kwenye mabano.

**PASIPOTI IMEPOTEA**

**ZUWENA ABDU ALI**
Anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE 355485**,iliyotolewa na Idara ya uhamiaji makao makuu Dar-Es-Salaam mwaka 2020.
Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kituo cha polisi chochote kilicho karibu.
**TAARIFA YA POLISI: MBE/MBE/RB/291635/2022**

RIPOTI MAALUM

# Miti inapokatwa kupisha mabango

Na Jenifer Gilla





Hali ya miti kabla na baada ya kukatwa ili kupisha matangazo katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, jijini Dar es Salaam.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

LICHA ya serikali na sekta binafsi kuhamasisha upandaji wa miti katikati ya maeneo mbalimbali ili kuhifadhi mazingira, uhifadhi huo umeonekana kuwa mtihani mgumu kwa baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Nipashe imeshuhudia ukataji wa miti iliyoko pembezoni mwa barabara ukifanywa kwa lengo la kuweka mabango ya matangazo.

Ni sura nyingine ya uharibifu wa mazingira na hata taswira yenyewe ya Mkoa wa Dar es Salaam, unaosifika kwa kuwa kitovu cha biashara nchini na Ukanda wa Afrika Mashariki.

Hivi karibuni Nipashe imeshuhuhudia ukatwaji wa miti iliyoko pembezoni mwa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, kipande cha kuanzia Mbuyuni hadi Bestbite wilayani Kinondoni, wakataji wakijikita kwenye lengo la kuyafanya mabango yao ya biashara yaonekane vizuri zaidi pasi na kujali athari kwa mazingira.

Mtaalamu wa Mazingira, Gwandumi Mwakatobe, anasema kukatwa kwa miti bila kufuata utaratibu maalum, kunasababisha athari kwa mazingira, binadamu na wanyama wengine, ikiwamo joto kali linalosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mwakatobe ana ufafanuzi zaidi kuhusu kadhia hiyo, akisema miti hasa sehemu ya majani inafanya kazi kubwa ya kusafisha hewa chafu inayozalishwa kutoka kwenye viwanda na moshi wa magari kwa kuwa inanyonya hewa hiyo na kumwepusha binadamu dhidi ya maradhi yatokanayo na uchafu huo.

"Pia kwenye miti tunapata vivuli na upepo wake husaidia kupunguza makali ya joto hasa huko Dar es Salaam, mnahitaji kuwa na miti mingi kwa sababu msimu wa joto huwa linakuwa kali sana. Kwa hiyo, serikali inaposisitiza upandaji wa miti, inakuwa na maana hiyo," Mwakatobe anasema.

Mkurugenzi wa Asasi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, anasema kuwa ili kudhibiti uharibifu wa mazingira mkoani Dar es Salaam, serikali inapaswa kushirikiana na wadau wengine kuja na msimamo mmoja utakaotumika kuongoza wawekaji mabango.

"Wadau kama Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), halmashauri, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Shirika la Umeme (TANESCO), wote wanahusika katika usimamizi wa miti iliyoko kando ya barabara, hivyo tukae pamoja tuweke mikakati ya pamoja ya kutunza miti hii,"anashauri.

### HATUA ZA KINONDONI

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Kinondoni, Shedrack Maximilian, katika ufafanuzi wake rasmi kwa Nipashe kuhusu kadhia hiyo, anasema wanafuatilia kwa ukaribu wanaokata miti bila kibali kando ya barabara katika manispaa na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika.

"Nimemtuma mtu wangu awatafute TANROADS ili wale wote waliokata miti hiyo ikibainika kuwa wamekata bila kibali, ni moja kwa moja faini, halafu tutahakikisha wanapanda miti," anasema.

Ofisa huo anasema kuwa ingawa wao siyo watoaji wa vibali vya kuweka mabango, wanatambua kwamba kitendo cha kukata miti kando ya barabara kina madhara kwa mazingira na wanyama na hawatokivumilia kwa sababu wanahusika na utunzaji wa mazingira katika manispaa hiyo.

"Haya maeneo ni ya TANROADS na TARURA, wao ndiyo wanaotoa kibali, lakini tumeshakaa na kukubaliana suala lolote linalohitaji ukatwaji wa miti barabarani, lazima watushirikishe ili tuone namna ya kufanya," anasema.

Pia anadokeza mpango uliopo wa kufanya sensa ya miti yote iliyoko katika manispaa hiyo na kuiweka namba ili iwe rahisi kugundua pale mti utakapokatwa.

"Ile miti mikubwa yote, hasa ya Msasani, Kinondoni na kuendelea, tunataka tufanyie sensa na tuiwekee alama za namba, halafu tunaweka vibao vya katazo la kukata mti. Ole wake atakakata mti," anaonya.

### USHIRIKIANO TANROADS

Nipashe inatua mezani kwa Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senkuku, kupata ufafanuzi wa hatua zinazochukuliwa kupiga vita uharibifu huo wa mazingira.

Senkulu anasema kwamba ili kudhibiti uharibifu huo, kunahitajika ushirikiano kati ya taasisi zote zinazohusika na uhifadhi wa barabara.

"Ninafikiri hilo ni suala la ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali kwa sababu taasisi yetu inashughulika na barabara na hifadhi ya barabara, lakini hatutoi rukhsa ya kukata mti.

"Tunahitaji kutambua eneo ambalo bango litawekwa na kumpa huyu mtu taarifa za ziada kwamba ukikuta kuna mti, siyo wa kwetu, wasiliana na mamlaka husika," anafafanua hatua zao.

Katika kuunga mkono jitihada za uhifadhi mazingira nchini, Senkulu anasema TANROADS imekuwa ikitoa elimu kwa wawekaji wa mabango hayo ili kuhakikisha wanaepuka kuwa sehemu ya wachafuzi wa mazingira.

Vilevile, Senkulu anasema wamekuwa wakihakikisha muundo wa mabango yanayowekwa barabarani, unaendana na taaluma ya uhandisi ili kuzuia majanga mbalimbali barabarani ikiwamo mabango kuanguka na ukatwaji wa miti.

### TFS KUJA NA SHERIA

Kwa sheria za uhifadhi nchini, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ndiyo wenye mamlaka ya kutoa vibali vya kukata miti nchini.

Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, katika mazungumzo mahsusi na Nipashe kuhusu kilichoshuhudiwa Kinondoni - miti kukatwa ili kupisha mabango ya matangazo, anasema kuwa wamepanga kukaa na mamlaka za Mkoa wa Dar es Salaam ili ziongeze vipengele katika sheria ndogo za mazingira.

Anasema sheria ndogo hizo zitawasaidia katika kusimamia utunzaji wa mazingira katika mkoa huo, ikiwamo kuzuia ukataji wa miti na uharibifu wa bustani zilizoko katikati ya miji.

Prof. Silayo anasema: "Pengine kinachowapa nguvu waharibifu hao ni kutokuwapo sheria ndogo ndani ya manispaa za kuwabana wale wote wanaoharibu mazingira pembezoni mwa barabara katika mkoa huo kama zinavyofanyika katika mikoa mingine.

"Sheria ya Misitu haizuii hii miti ambayo ipo huku mijini kwenye maeneo ambayo ni miundombinu mingine, lakini inaruhusu halmashauri kutengeneza sheria ndogo na kubana sasa katika maeneo yake.

"Tuna sheria inayomkataza mtu kukata miti kwa ajili ya matumizi fulani, lakini kwenye ngazi hizi za chini, kwa mfano kwenye halmashauri na jiji, kuna halmashauri ambazo tumekubaliana nazo na zikaweka sheria ndogo kama vile mkoa mzima wa Kilimanjaro. Bado hatujawa na sheria ndogo za kudhibiti hali hiyo kwa hapa Dar es Salaam," anakiri.

Prof. Silayo anarejelea Sheria Ndogo za Mabango na Matangazo ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za Mwaka 2016, akijikita zaidi kwenye kifungu cha 15 ambacho anasisitiza kinasaidia kutunza mazingira kwenye mkoa huo.

Kwa kuirejea sheria tajwa, kifungu hicho kinasema: "Mtu yeyote, kwa uzembe au makusudi, hataruhusiwa kuharibu mazingira na mali nyingine wakati wa kuweka, kujenga au kuondoa bango au tangazo lake."

### KAULI YA WIZARA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, katika mazungumzo na Nipashe kuhusu kadhia hiyo wiki iliyopita, alisema vitendo vya ukatwaji miti hiyo hakikubaliki kwa sababu kinakwenda kinyume cha maagizo ya serikali na kurudisha nyuma juhudi za mkoa kuhifadhi mazingira.

"Tumeshuhudia hivi karibuni katika mkoa mfano wa Dar es Salaam, kuna vitendo vya kukata matawi ya miti kwa ajili ya matangazo mbalimbali ya wafanyabiashara.

"Sasa hii haikubaliki. Ni jukumu la kila mfanyabiashara kuhakikisha anaweka tangazo lake eneo ambalo wateja wake wataliona bila kuathiri mazingira," Dk. Jafo aliagiza.

Alisema kwa sasa ajenda ya utunzaji mazingira ni endelevu na wanaendelea na kampeni ya upandaji miti inayoitwa 'Mazingira Yangu, Tanzania Yangu Naipenda Daima', yenye lengo la kuhamasisha wanafunzi na kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5, yaani miti milioni 276 Tanzania nzima.

"Ni juzi tu nilikuwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam (Amos Makalla) ambaye amenithibitishia kuwa anaanza mkakati kabambe wa kuhakikisha Dar es Salaam inakuwa nadhifu pamoja na kupendezesha eneo lote kuanzia (uwanja wa ndege) mpaka katikati ya Jiji la Dar es Salaam," alisema.

Dk. Jafo alisema msimamo wa ofisi yake ni wadau wote kushirikiana na serikali kutunza mazingira na pia kama kuna mfanyabiashara anataka bango lake lionekane vizuri, aweke bango ambalo halitaathiri mazingira ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo ni janga kubwa kwa sasa duniani.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Tanzania inakabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika maeneo mengi ya nchi, kukiwa na ongezeko la nyuzi joto 10 kulingaishwa na miaka ya 1960.

Ofisi hiyo pia inabainiha kuwa athari zinazolipata Jiji la Dar es Salaam ni pamoja na kina cha maji ya bahari kuongezeka kwa kiwango cha 0.492 sawa na mm 6 kwa kipindi cha miaka 16 kuanzia mwaka 2002 hadi 2018, hali inayosababisha mmomonyoko wa fukwe na uharibifu wa mazingira.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi, Dk. Hilideltha Msita, alipokagua ujenzi wa kiwanda hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mume, mke wateketea moto

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watatu wamefariki dunia katika matukio mawili tofauti, likiwamo la mume na mke kuteketea kwa moto wakiwa wamelala ndani ya nyumba yao na mwingine mwenye tatizo la kifafa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mark Chilya, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo mwishoni mwa wiki, katika kata za Mihumo na Likongowele, wilayani Liwale, mkoani humo.

Aliwataja waliofariki kuwa ni Bakari Saidi (30), mkazi wa kijiji cha Likombora, Jafari Libaba (45) na mpenzi wake aliyefahamika kwa jina moja la Esther, wakazi wa Kata ya Likongowele.

Akielezea matukio hayo, alisema Bakari alikuwa anasumbuliwa na kifafa na ugonjwa wa kifua kikuu (TB), ambaye mwili wake ulikutwa pembezoni mwa viwanja vya Shule ya Msingi Liwale Mjini.

Alisema Libaba na Esher wamepoteza maisha kwa kuteketea kwa moto wakiwa ndani ya nyumba yao wamelala na mume alikufa papo hapo na mke alifia hospitalini akipatiwa matibabu. "Ni kweli taarifa hizo zipo mezani kwangu na mwili wa Bakari umekutwa maeneo ya Shule ya Msingi Liwale mjini," alisema Chilya.

# Bilioni 1.1/- zakusanywa kampeni kukabili UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), imeendelea kuweka rekodi katika utoaji wa huduma za kijamii baada ya kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.1 kupitia kampeni ya GGM Kili Challenge 2022 iliyoanza Juni 29 na kuhitimishwa Julai 21, mwaka huu.

Kampeni hiyo iliyoasisiwa na GGML miaka 20 iliyopita, ni mahsusi kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu VVU/UKIMWI pia kuchangisha fedha za udhibiti wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa lengo la kusaidia jitihada katika serikali kufikia sifuri tatu kwa maana ya kutokomeza maambukizi mapya kwa kufikia asilimia sifuri, sifuri ya unyanyapaa na sifuri katika vifo vitokanavyo na UKIMWI.

Akizungumza mwishoni mwa wiki iliyopita wilayani Moshi katika hafla ya mapokezi ya washiriki 52 waliopanga Mlima Kilimanjaro, Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simona Shayo, alisema kampeni ya mwaka huu imekuwa na mafanikio ya kipekee.

Makamu wa Rais alibainisha kuwa kati ya wapandaji mlima hao, 24 walipanda Mlima Kilimanjaro kwa kutembea kwa miguu na 28 kwa kuuzunguka kwa kutumia baiskeli kupitia lango la Machame na kushukia Mweka.

Alisema kampeni hiyo iliyozinduliwa rasmi Juni 29 jijini Dodoma na kufuatiwa na harambee ya uchangiaji fedha iliyofanyika Julai 14 kisha Julai 15 washiriki wakaagwa kwa ajili ya kupanda mlima, pia ilijumuisha utoaji wa huduma bila malipo ya upimaji wa VVU na kisukari na utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa wakazi wa Mji wa Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Alisema huduma hizo zilitolewa katika lango la Machame, Kialia, Soko la Kalali, Nshara na Mweka.

"Ni furaha kubwa kuwaeleza kuwa katika huduma hizo zilizoanza kutolewa kuanzia tarehe 15 hadi 18 Julai mwaka huu, jumla ya watu 463 wamepimwa VVU ambapo wote majibu yameonyesha hawana maambukizi ya VVU.

"Vivyo hivyo, watu 411 wamejipima wenyewe kwa hiari. Hii ni hatua kubwa katika mwitikio wa Watanzania kutaka kujua hali ya afya zao," alisema.

Pia alisema katika utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19, wataalamu wamefanikiwa kuchanja watu 822 ambao kati yao, wanaume ni 365 na wanawake ni 427 wakati katika uchangiaji wa damu zimekusanywa chupa au unit 27 za damu huku katika ugawaji wa kondomu, jumla ya mipira ya kiume 9,335 na ya kike 200 iligawiwa katika maeneo hayo. "Pia ili kutoa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI, tembe za PrEP ambazo ni mahsusi kwa matumizi ya kupunguza makali ya VVU na kwa watu waishio na VVU ili kuzuia upatikanaji wa maambukizi ya VVU ziligawiwa pamoja na vipeperushi 204 vya masuala ya afya ya uzazi," alisema.

Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema fedha zilizokusanywa kwenye kipindi cha kampeni hiyo kwa ujumla ni Sh. bilioni moja.

Pia alitoa wito kwa wadau wengine kukaa mezani na taasisi hiyo ili kupeana mbinu za kuchangisha fedha zaidi kutunisha mfuko wa udhibiti UKIMWI nchini.

Akizungumza katika mapokezi hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, aliwapongeza washiriki hao 52 wa waliopanda Mlima Kilimanjaro na kuwaita kuwa ni mashujaa.

Akizungumzia matokeo ya vipimo vya VVU kwa watu zaidi ya 400, Kagaigai alisema yanaonyesha jinsi gani mapambano wanayofanya kukabiliana na VVU sasa yanaelekea kwenye mafanikio. Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, pia alipongeza juhudi zilizoonyeshwa na GGML na wadau wake na kusema kuwa matokeo ya vipimo hivyo yanaonyesha dhamira ya serikali kufikia sifuri tatu inakwenda kutimia.

Alionya dosari iliyobaki ni ya maambukizi mapya kwa kuwa waathiriwa wengi hawapotezi maisha kwa VVU au hawaonyeshi dalili.

Mmoja wa wapandaji mlima huo, Lucina Livigha, alisema licha ya vikwazo kadhaa katika upandaji wa mlima, wamejiona fahari kuwa sehemu ya mafanikio ya kampeni hiyo inayookoa

# Wasomi wanavyouzungumzia uchumi wa buluu visiwani

**Na Mary Geofrey**

WASOMI na wataalamu wa uchumi nchini wamesema mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga uchumi wa buluu, utaupaisha uchumi na maendeleo ya visiwa hivyo kwa haraka.

Tangu alipoingia madarakani mwaka 2020, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Mwinyi, alisema serikali itatumia fursa zinazozunguka visiwa hivyo zikiwamo fukwe, uvuvi, kilimo cha mwani sambamba na mazao ya baharini.

Mmoja wa wataalamu wa uchumi na uwekezaji, Sadiki Mbarouk Mahamudi, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, alitaka wananchi wahamasishwe kufahamu fursa hizo na namna taifa linavyoweza kunufaika.

"Zanzibar imebarikiwa kuwa na fukwe nyingi ambazo ni nzuri kwa uwekezaji wa mahoteli na vivutio mbalimbali kwa utalii. Kinachotakiwa hapa uungaji mkono wa Wazanzibari wote katika kufanikisha hili," alisema Mahamudi.

Kadhalika, alisema fursa zinazoizunguka Zanzibar ni nyingi na kuipongeza serikali kwa kuliona hilo katika awamu ya uongozi uliopo.

Mhadhiri wa Sheria Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya, Dk. Tasco Luambano, alisema uamuzi wa Rais Mwinyi kuunda wizara maalumu inayoshughulikia masuala ya uchumi wa buluu unatoa tafsiri halisi ya maono ya kiongozi huyo katika kuiletea Zanzibar mageuzi stahiki ya kiuchumi.

"Hatua ambazo Rais Mwinyi amezichukua tangu aingie madarakani zimelenga kuibadilisha na kuipaisha Zanzibar kiuchumi na kimaendeleo. Mwenye macho hapaswi kuambiwa aone kwani Zanzibar ya 2020 siyo ya 2022," alisema.

Dk. Luambano alipongeza juhudi anazochukua Rais Mwinyi kuhakikisha kuwa mazao na rasilimali zinazotokana na bahari zinatumika kuijenga Zanzibar na kuwaletea wananchi maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Dk. Zubeda Salim Abdallah, alisema uchumi wa buluu ni njia sahihi ya kujenga uchumi imara kwa Zanzibar kwa sababu kupitia mazao ya bahari, uvuvi na rasilimali zote zinazovizunguka visiwa hivyo maisha ya Wazanzibari wote yatabadilika kwa haraka.

"Uchumi wa buluu ni msingi wa kujenga sekta zingine za uchumi zikiwamo utalii na huduma za kijamii, viwanda, miundombinu, mawasiliano, elimu, afya na nyingine nyingi," alisema Dk. Zubeda.

Hivi karibuni, viongozi wastaafu walikemea habari za upotoshaji kuwa Rais Mwinyi ameuza visiwa kama sehemu ya kumkatisha tamaa na juhudi za serikali yake kuhamasisha uwekezaji kwenye fukwe ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwenye michezo ya madola tutavuna kile tulichopanda

**MICHEZO** 18 ya Jumuiya ya Madola inafanyika jijini Birmingham nchini England kuanzia Julai 28 hadi Agosti 8, mwaka huu na Tanzania ni miongoni mwa nchi zitakazoshiriki michezo hiyo.

Tanzania katika michezo hiyo itawakilishwa na timu za michezo ya riadha, ndondi, judo na kuogelea na kwa mara ya kwanza kutakuwa na mchezo wa kunyanyua vitu vizito kwa wenye ulemavu.

Kwa miaka mingi Tanzania imekuwa ikifanya vizuri katika michezo hiyo, lakini miaka inavyozidi kwenda mbele, matokeo yetu yamekuwa sio mazuri na katika michezo mitatu iliyopita ya Madola, wachezaji wetu wamerudi mikono mitupu.

Hadi sasa Tanzania ina jumla ya medali 21 za aina mbalimbali kutoka katika Michezo ya Jumuiya ya Madola, ambapo medali za dhahabu ni sita, fedha sita na shaba zikiwa tisa.

Ukiangalia historia, nyingi ya medali hizo Tanzania ilizotwaa zimetokana na mchezo wa riadha pamoja na ngumi. Tanzania ilianza kushiriki michezo hiyo mwaka 1966 Kingstone, Jamaica kabla ya kushiriki mwaka 1970 huko Edinburgh, ambako tulitwaa medali moja ya shaba.

Katika historia ya Tanzania kushiriki Michezo ya Jumuiya ya Madola, kipindi kizuri zaidi kilikuwa mwaka 1974 michezo hiyo ilipofanyikia Christchurch, New Zealand ambako Filbert Bayi alivunja rekodi ya dunia na ile ya Jumuiya ya Madola.

Bayi alivunja rekodi ya dunia ya mbio za mita 1,500 baada ya kutumia dakika 3:32.16 na ile ya Jumuiya ya Madola ambayo hadi sasa anaishikilia ikiwa ni miaka 48 imepita tangu aitwae medali hiyo.

Mbali na Bayi, baadhi ya wanariadha wengine waliotwaa medali katika Michezo ya Jumuiya ya Madola ni pamoja na Samson Ramadhani, Francis Naali, Simon Mrashani na wengine.

Timu ya Tanzania mwaka huu inakwenda Birmingham, kushiriki michezo hiyo, huku kukiwa na matumaini makubwa ya kurudi na medali baada ya miaka 12 ya kutoka kapa.

Baada ya riadha kwa muda mrefu kupeleka wakimbiaji wa mbio ndefu, mwaka huu timu ya Tanzania ina wachezaji wa mbio fupi kama mita 100, 200 na zile za kati za mita 800 na 1,500 pamoja na ndefu za uwanjani za mita 5,000 na 10,000.

Kwa upande wa mbio fupi, matumaini ni madogo ya kurudi na medali kwani wanariadha wetu hawajapata uzoefu wa kutosha katika kada hiyo, tofauti na wale wa marathoni, ambao angalau wameshiriki mbio nyingi na kufanya vizuri, mfano Simbu.

Mfano hai ni baadhi ya wanariadha wetu wa mbio fupi, walishiriki mashindano nchini Kenya, lakini walishindwa kung'ara, hivyo hata nafasi ya kufanya vizuri katika Michezo ya Jumuiya ya Madola inawezekana isiwepo.

Hivyo, sisi tunasema kwamba, maandalizi yaliyofanyika kuelekea michezo hiyo ndio yatakayotoaa taswira ya namna gani wanamichezo wetu wanaweza kurudi na medali.

Pamoja na yote tunaamini kwamba, maandalizi waliyofanya yanaweza pia kuwafanya wakarudi na medali, ingawa kazi sio ndogo na sisi kama wadau wa michezo tunawatakia kila la heri.






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusiibeze Stars, wachezaji hawako fiti

Na Adam Fungamwango

**NIMEONA** mahali mashabiki na wachambuzi wakibishana kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kiwango cha Taifa Stars dhidi ya Somalia juzi.

Baadhi wanasema kuwa Stars haikucheza kwenye kiwango cha kuridhisha ambacho wao walitarajia.

Wakasema timu kama ya Somalia ambayo kwao hata ligi yenyewe inacheza kwa mashaka mashaka, ilitakiwa Stars ishinde idadi kubwa ya mabao pamoja na kutawala mpira.

Wapo waliohoji kwa kiwango kile na matokeo ya kushinda bao 1-0 kwa tabu, ni kwamba kiwango cha Stars kimeshuka au Somalia wamepandisha kiwango chao ndiyo maana mechi ilionekana ngumu kivile?

Stars ilishinda bao 1-0 kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani (CHAN), ikipigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo kikanuni Somalia ilihesabika kuwa ipo nyumbani, kwani ilichagua uwanja huo kutokana na nchini kwao kutokuwa kwenye hali ya usalama.

Lilikuwa ni bao pekee lililofungwa na Abdul Selemani 'Sopu' dakika moja baada ya mapumziko, akiruka juu na kuunganisha kwa kichwa mpira wa krosi kutoka kwa Kibwana Shomari.

Kwanza kabisa waliokuwa wanadhani Stars ingeweza kushinda mabao mengi kwa timu ya Somalia kwa sababu ni dhaifu si kweli.

Rekodi zinaonyesha kuwa timu hizo zimekutana mara 10, lakini kati ya hizo licha ya kwamba Stars imeshinda mara nane, lakini si kila zinapokutana inapata ushindi mnono, hata nyakati ambazo ilikuwa na kiwango bora.

Imewahi kuishinda mabao mengi mara mbili tu, mwaka 1995 na mwaka 2012, iliposhinda mabao 7-0 kwenye kila mechi kati ya hizo mbili.

Mwaka 1980 Stars ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Somalia na 2009, Somalia iliinyuka Stars bao 1-0, michuano yote tisa ikiwa ni ya Kombe la Challenge, kasoro mechi ya juzi ambayo ni ya CHAN.

Hii inaonyesha kuwa pamoja na kwamba Somalia inaonekana ni kibonde, lakini si kihivyo.

Kingine ni kwamba nilivyoangalia mechi ile nilichogundua ni kwamba wachezaji wengi wa Stars walikuwa wazito, wavivu na walikuwa hawafiki maeneo husika kwa wakati.

Halafu kila muda unavyozidi kwenda walionekana kuchoka kuliko wenzao na dakika za mwisho walisukuma mashambulizi kiasi kwamba ilibaki kidogo isawazishe kama si umahiri wa kipa Aishi Manula na kusababisha hata kuumia.

Hii ilisababishwa na kwamba wachezaji wengi wametoka majumbani. Wengi 'wakula sana bata' na sasa wameanza kurejea kwenye timu zao kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Hebu angalia, Simba kwa sasa inaingia kwenye wiki ya pili ya maandalizi ya msimu nchini Misri, Azam ipo kwenye wiki ya kwanza, Yanga ina siku chache tu tangu ianze kambi, na timu zingine ndiyo kwanza zimewaita wachezaji wao kwa ajili ya kuanza msimu mpya.

Na baadhi ya wachezaji ndiyo hawahawa ambao wapo kwenye kikosi cha timu ya taifa, hivyo wala kwangu mimi nisingetegemea makubwa sana.

Hiki ni kipindi ambacho makocha huwafanyika kwanza wachezaji mazoezi magumu kuwaweka fiti kwani wengine wanakuwa wamekula vyakula vya mafuta au kula bila mpangilio kiasi kwamba wamenenepa, lakini wanakosa pumzi kwa sababu ya kukaa muda mrefu bila mazoezi, hivyo kuchoka haraka.

Watanzania wanapaswa kushukuru hata hilo bao moja lililopatikana kwani kucheza kwenye mazingira ya aina hiyo inakuwa ni ngumu mno.

Na ndiyo maana wachezaji wengi hawakuwa kwenye viwango vya kawaida. Kuanza kuwalaumu au kuwaponda ni kutowatendea haki.

Wachezaji walicheza bila mazoezi na timu ya taifa ambayo wachezaji wao wengi hawatoki Somalia, kwani wanaishi nchini Kenya na kwa sababu wao hawakuwa na ligi, walikuwa wakicheza soka kwenye michuano mbalimbali.

Cha kushukuru ni kwamba hatukupangiwa na timu ngumu sana kwani hali ingekuwa mbaya. Iwapo itaiondoa Somalia, itacheza na Uganda. Nadhani wakati huo tayari wachezaji wanakuwa wamechanganya, kwani wengi watakuwa wamekwenda kwenye klabu zao na kufanya mazoezi ya mwanzo wa msimu ambao yatawafanywa wawe fiti.

Wakati mwingine Watanzania tuache tabia ya kubeza vitu bila sababu ya msingi au kuuliza kwanza.

Tusubiri kwanza wachezaji wetu wawe fiti ndiyo tuangalie kama wataendelea kucheza hivi au watabadilika ndiyo tuanze kuhoji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda, Exaud Kigahe (wa pili kushoto walioketi), akiwa na waandaaji wa tuzo za masoko 2022 kutoka Chama cha Sayansi ya Masoko Tanzania (TMSA) katika utoaji tuzo hizo kwa washindi kutoka vipengele 14, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam, juzi. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya TMSA, Dk. Emmanuel Chao na kulia walioketi ni Yusuph Kashindi Zubeir (Mratibu Mkufunzi TMSA) na Dk. Salama Yusuf (Mwenyekiti TMSA Zanzibar). Nyuma waliosimama ni maofisa wa TMSA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi za kodi ya pango la ardhi zakwama ushahidi

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

KESI 107 za kodi ya pango la ardhi katika Mkoa wa Singida zimekwama kuendelea katika Baraza la Ardhi na Nyumba kutokana na maofisa ardhi waliozifungua kushindwa kufika kwenye baraza hilo kutoa ushahidi.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Singida, Bahati Colex, alisema hayo juzi wakati wa kikao kazi cha watumishi wa sekta ya ardhi kutoka katika halmashauri za Mkoa wa Singida kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli zilizofanyika katika kipindi cha 2022/2022.

Alisema maofisa ardhi kutoka halmashauri za Mkoa wa Singida wanafungua kesi za pango ya ardhi, lakini wanapoitwa na Baraza la Ardhi na Nyumba hawafiki na ku kwamisha kutolewa hukumu ya kesi hizo kwa muda mrefu.

"Asilimia kubwa ya kesi za ardhi ndiyo wanakuwa mashahidi, lakini bahati mbaya hawafiki na tunajikuta kesi nyingi tunaziweka pending (pembeni)," alisema.

Colex alisema katika Baraza la Ardhi na Nyumba zipo jumla ya kesi 515 za ardhi ambazo zinasubiri utatuzi na nyingine zilifunguliwa tangu mwaka 2014.

Alisema sababu ya kesi hizo kuchelewa kutolewa uamuzi ni uchache wa watumishi, waliopo ni watatu pekee kati ya sita wanaohitajika, changamoto ya usafiri, baraza kukaa miaka miwili bila kuwa na mwenyekiti na baadhi ya kesi kurejeshwa kutoka Mahakama Kuu kwenda kwenye baraza.

Naye Ofisa Utumishi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Salum Issa, alisema changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya ardhi inafanyiwa kazi.

Issa alisema kuwapandisha vyeo watumishi limekuwa tatizo kwasababu wengi mafaili yao hayana nyaraka na vyeti vyao.

"Wapo watumishi karibu 160 ambao tumeshindwa kuwapandisha vyeo kwasababu nyaraka zao hazipo kwenye mafaili," alisema.

Aidha, Ofisa Utumishi huyo aliwataka maofisa ardhi kuweka masanduku ya maoni kwenye ofisi ili wananchi waweze kutoa maoni.

# Shule zajengewa vyoo, msaada madawati

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Knauf imetoa msaada wa madawati 300, kujenga matundu 10 ya choo na chumba kimoja cha darasa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 60 katika Shule ya Msingi Kisemvule na Mwanambay, Mkuranga mkoani Pwani.

Ni mara ya pili mwaka huu kampuni hiyo inayojihusisha kutengeneza na kuuza vifaa vya ujenzi, kusaidia elimu baada ya shule za Makangaga na Kiranjeranje zilizoko Kilwa, mkoani Lindi.

Akiongea baada ya kukabidhi misaada hiyo, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Ilse Boshoff alisema, kusaidia maendeleo ya elimu katika jamii ni moja kati ya vitu wanavyovipa kipaumbele muhimu.

"Kuwajengea watoto mazingira bora ya kujifunzia ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote. Kila mwanafunzi ana haki ya kupata elimu bora na Knauf tunayo furaha kubwa kusaidia maendeleo ya elimu hapa Tanzania kwani jambo sahihi na muhimu," alisema.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Kata, Shizya Mwaweza, alisema msaada huo umesaidia kuongeza mahudhurio ya wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 90.

"Baada ya kupata msaada wa madawati haya pamoja na vyoo, mahudhurio yameongezeka kwa asilimia 90 hadi 95. Hii ni kwa sababu mazingira yao ya kujifunzia yameboreshwa na wanafurahia kuja shuleni," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, Veronica Kinyemi, alisema madawati hayo yatasaidia wanafunzi 900 kuketi wakisoma na kusaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia.

# TEN/MET yaipongeza serikali kuboresha elimu

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TEN/MET), umeipongeza serikali kwa maboresho kwenye sekta ya elimu nchini.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Taifa wa Mtanda huo, Ochola Wayoba, hatua zinazochukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha sera, sheria na mitaala katika sekta hiyo ni jambo jema na linatakiwa kuungwa mkono.

"Uwekezaji unaofanyika kwenye sekta ya elimu, 'review' (mapitio) ya sera, sheria, mitaala na maboresho mbalimbali, tunaona hiyo ni nia njema ya serikali kwenye sekta hii na tunaiomba iendelee kuboresha zaidi kuhakikisha inaendana na mahitaji ya sasa ya dunia," alisema Wayoga.

Alisema, wanaamini katika maboresho hayo yanayofanywa na serikali, itaangaza zaidi kuhakikisha uwekezaji katika sekta hiyo ya elimu inakidhi mahitaji ya sasa ya kitaifa na kimataifa, ili wanafunzi wanaohitimu wawe na maarifa ya kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

"Tunaamini kwamba mitaala inayofanyiwa maboresho kwa sasa itakuwa ni ile ambayo inalenga kuwatengeneza wanafunzi ambao wakihitimu wanakwenda kutengeneza kitu, kwa sababu tunaona wanafunzi wengi wanahitimu, lakini hawajianzishii shughuli za kufanya, hatutaki kuendelea kuona wanatoka shuleni wanakwenda kuwa wategemezi wa wazazi wao," alisema Wayoga.

Pia alisema pamoja na maboresho ambayo serikali inafanya katika sekta hiyo ya elimu, bado kuna upungufu kwenye eneo la walimu pamoja na ukosefu wa miundombinu bora.

"Kwa hiyo katika kipindi hiki cha maboresho ni vema serikali ikaliangalia hili hususani kuwekeza kwenye miundombinu ikiwamo vifaa, teknolojia za kisasa za kufundishia na sekta hii iongezewe bajeti," alisema Wayoga.

Suala jingine ambalo walitaka liangaliwe wakati wa maboresho hayo ni uendelezaji wa walimu, na kwamba ni vyema sera ya elimu ikatamka wazi juu ya suala hilo.

Pia alipendekeza lugha ya kujifunzia itumike Kiswahili na Kiingereza ili elimu inayotolewa ikidhi mahitaji ya ndani na kimataifa.

"Tunaamini kwamba endapo lugha ya kujifunza itakuwa Kiswahili na Kiingereza, itasaidia kutoa wanafunzi ambao watatumika ndani na nje ya taifa hili, wataendana na dunia inavyokwenda kwa kutumika kimataifa," alisema Wayoga.

# Makarani sensa wahamasisha watu kuhesabiwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya makarani wakufunzi ngazi ya wilaya mkoani Kagera, wamesema maendeleo chanya yanatokana na usahihi wa taarifa za sensa zitakazokusanywa wananchi watakapohesabiwa.

Walikuwa wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, ikiwa ni siku ya 17 tangu kuanza kwa mafunzo ya uadilifu wa kuwa wakufunzi wa makarani watakaofanyakazi kwenye kata.

Mkufunzi mkazi wa Wilaya ya Muleba, Jackson Msigati, alisema wameaminiwa kufundisha wengine ngazi ya kata, ili kuhakikisha takwimu sahihi za waliohesabiwa zinapatikana.

"Niseme tu maelekezo yote ambayo tumepewa ni kuhakikisha taarifa zote za sensa zinakuwa na usahihi wake na serikali itumie namba kufanya maendeleo," alisema Msigati.

Alisema sensa ifanyika kila baada ya miaka 10, kwa lengo la kujua idadi ya watu kwa ajili ya kupanga mipango sahihi kwa maendeleo jumuishi.

Karani na mkazi wa Kata ya Kagondo Manispaa ya Bukoba, Jane Novath, alisema elimu ya utambuzi inajengwa kwa makarani itafikia wananchi kwa kufuata miongozo ya madodoso kwa nadharia na vitendo.

Naye Ofisa TEHAMA, Elikana Joseph, alisema mwaka huu sensa itafanyika kidigitali na taarifa zitawasilishwa kwa mtandao kufika mahali pa kujumuisha.

Naye Mkufunzi wa Sensa Taifa, Morice Nyatega, alisema kinachofanyika sasa ni mafunzo ya uelewa kwa makarani wakufunzi watakaokwenda kufundisha wengine ili kuwa na weledi kwenye ukusanyaji wa taarifa zote.



Meneja Idara ya Mauzo wa Kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited, Stephen Godfather, akifafanua jambo kwa viongozi na wakulima 120 wa zao la tumbaku kutoka Sikonge mkoani Tabora na Kahama walipofanya ziara katika kiwanda hicho kilichoko Kingolwira mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima ufuta wapata mamilioni uuzaji zao hilo

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya kilo 25,001,222 za ufuta sawa na tani 25,000 zimekusanywa na kuuzwa na Chama Kikuu cha Ushirika mkoani humo, kupitia minada sita iliyofanyika msimu wa mauzo wa mwaka huu na kuingiza mamilioni ya maduhuri.

Meneja wa Chama hicho kinachoundwa na halmashauri za Kilwa, Lindi na Mtama, Nurdini Swalah, alisema hayo katika mahojiano maalumu na mwandishi wa habari hizi, mjini hapa.

Alisema katika minada sita iliyofanyika Vyama vya Msingi na Ushirika (Amco's) za Tapwa, Nakiu, Halmashauri ya Kilwa na Milola, Kiwalala na Nyangamara (Mtama) imeingiza Sh. 79,354,800,353, huku wakulima wakiweka kibindoni Sh. 77,052,187,309.

Alifafanua kuwa mnada wa kwanza kilo zilizouzwa ni 4,152,224 na kuingiza maduhuri ya Sh. 12,917,217,587/50, wakati wa pili kilo zilizouzwa ni 4,331,085 na kuingiza Sh. 13,520,040,500/50 na watatu kilo 4,795,397 zimekusanywa na kuingiza Sh. 15,000, 795,207/50. Aidha, alisema katika mnada wa nne kilo zilizokusanywa na kuuzwa zilikuwa 4,110,445 na kuingiza Sh. 13,226,042,687/50, wa tano kilo 4,719,250 zilikusanywa na kupata Sh. 15,300,906,723, wakati mnada wa sita ukiingiza Sh. 9,399,697,656/50 baada ya kuuza kilo 2,892,821.

Meneja wa Chama Kikuu cha Lindi Mwambao, alisema uuzaji wa ufuta kupitia minada hiyo sita, Sh. 2,312,612,253/70 ni makato na tozo mbalimbali, Sh. 1,750,085,554 usafirishaji, Sh. 37,501, 033/50 zinatokana na maghala, wakati vifungashio vikilamba Sh. 525,025, 666/20.

Kutokana na mauzo na makato yote yaliyofanyika, wakulima wamelipwa Sh. 69,965,102,707 huku minada ikiendelea kuonyesha kiwango kikubwa cha ufuta uliozalishwa msimu wa mwaka huu.

Swalah alisema kutokana na kiwango cha ufuta uliozalishwa na kuuzwa msimu wa mwaka huu, yapo matumaini ya kufanya vizuri, ikiwamo kiwango cha idadi ya zao hilo, kupita cha uzalishaji wa mwaka uliopita, hadi msimu unamalizika mwaka jana, Chama cha Lindi Mwambao kilikusanya na kuuza kilo 27,000,0000.

# Tunduru yaongoza ukusanyaji korosho 2021/22

**Na Gideon Kwakanosya, TUNDURU**

CHAMA cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) Namitili kilichoko Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, kimeshika nafasi ya kwanza kitaifa kwa kuongoza ukusanyaji korosho katika msimu wa mwaka 2021/2022.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, Asangye Bangu alisema, katika kipindi hicho Namitili AMCOS ilikusanya korosho zenye uzito wa kilo 1,879,635 na kuongoza katika kumi bora kitaifa.

Akizungumza na wakulima na wanachama wa Namitili AMCOS, alisema nchini kuna zaidi ya AMCOS 400 ambazo zinakusanya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Aliitaja AMCOS iliyoshika nafasi ya pili kuwa ni Sama kutoka Wilaya ya Tunduru ambayo imekusanya korosho kilo 1,774,676, na nafasi ya tatu ni Umoja AMCOS kutoka Wilaya ya Liwale mkoani Lindi ambayo imekusanya kilo 1,758,118.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, nafasi ya nne imekwenda kwa Tuaminiane AMCOS kutoka Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara iliyokusanya kilo 1,656,787, nafasi ya tano imechukuliwa na Lima AMCOS kutoka Wilaya ya Tunduru, ambayo imekusanya kilo 1,461,614 ambapo nafasi ya sita imeenda kwa Kitangari AMCOS kutoka Wilaya ya Newala mkoani Mtwara iliyokusanya tani 1,297,637.

Aliitaja AMCOS iliyoshika nafasi ya saba kuwa ni Nanyumbu Mangaka kutoka mkoani Mtwara, ambayo imekusanya kilo 1,222,606, nafasi nane imeshikwa na Nangoo AMCOS toka Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara iliyokusanya kilo 1,174,361.

AMCOS nyingine zilizoingia kumi bora ni Chapakazi ya Kibiti mkoani Pwani iliyokusanya kilo 1,111,733 na nafasi ya kumi bora imechukuliwa na Mayanga AMCOS ya mkoani Mtwara ambayo imekusanya kilo 1,110,449.

Akizungumza na wanachama wa Namitili AMCOS, Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa stakabadhi ghalani ameipongeza AMCOS hiyo kushika nafasi ya kwanza kitaifa na kusisitiza kuwa wamelifanya kitaifa na nafasi wameipata kihalali kulingana na vigezo vilivyowekwa.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU), Musa Manjaule, alisema Tunduru inajivuna kwa kutoa AMCOS tatu bora kitaifa nafasi ya kwanza, pili na tano zimechuliwa na AMCOS za Tunduru.

Alisema Wilaya ya Tunduru imepiga hatua kubwa katika matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye mazao ya korosho, ufuta na mbaazi.

Ameutaja mfumo huo tangu ulipoanza kutumika msimu wa mwaka 2015 hadi sasa umeleta manufaa makubwa kwa wakulima.

Kwa upande wake mkulima Ibrahimu Chemba, mwanachama wa Namitili AMCOS, alizitaja sababu zilizochangia AMCOS hiyo kupata mafanikio makubwa ni uwapo wa viongozi mahiri wanaofanya kazi za wanachama kwa moyo, uwazi wa wanachama na kuwapo kwa makarani waaminifu.

## Wilaya Iramba yakomesha mimba, ukeketaji shuleni

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

WILAYA ya Iramba mkoani Singida, imekomesha vitendo vya wanafunzi wa kike kupewa mimba, ukeketaji na kuozwa wakiwa na umri mdogo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Suleiman Mwenda, alisema hayo jana kwenye hafla ya Siku ya Kitaaluma ya Shule ya Sekondari Tumaini na wanafunzi na walimu waliofanya vizuri kwenye masomo walipewa zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu.

Mwenda alisema wilaya hiyo kila mwezi kulikuwa kukiripotiwa wanafunzi wanane hadi tisa kupewa mimba, lakini hivi sasa matukio hayo hakuna baada ya serikali kuanza kuwachukulia hatua kali za kisheria waliokuwa wakifanya vitendo hivyo.

"Wakati naingi hapa Iramba nikiwa DC kila mwezi kwenye taarifa ya kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama tulikuwa tunaletewa taarifa za mimba nane hadi tisa kila mwezi, lakini hivi sasa ni miezi minne hakuna mimba ambayo imeripotiwa katika shule zetu za sekondari," alisema.

Alisema serikali ya wilaya ilipoona tatizo la mimba, ukeketaji na kuoza watoto limekuwa sugu, iliweka mkakati wa kukomesha vitendo hivyo kwa kuwachukulia hatua wote waliokuwa wakishiriki vitendo vya ngono na wanafunzi na wengi wamefungwa jela miaka 30.

Alisema serikali imechukua hatua hiyo ili kutengeneza mazingira mazuri kwa wanafunzi wa kike waweze kusoma ili baadaye wawe na maisha mazuri na kuwa viongozi bora wa taifa kwa kuwa inaaminika wanapopewa nafasi za uongozi wanafanya vizuri zaidi kuliko mwanaume.

Mwenda alisema serikali imeendelea kuchukua hatua ya kuboresha mazingira ya Shule ya Sekondari Tumaini na katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022, shule hiyo ilipatiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya kujenga mabweni, madarasa na kuyaboresha madarasa yaliyopo.

Alisema Benki ya NMB katika kuunga juhudi za serikali imetoa vitanda 40 vya wanafunzi 80 wa shule hiyo ambayo kila mwaka imekuwa ikifanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha pili, nne na sita na kuibeba wilaya na mkoa wa Singida.

Vile vile, serikali katika kugharamia elimu bure Wilaya ya Iramba inapewa Sh. milioni 654 kwa shule za sekondari na Sh. milioni 403 kwa shule za msingi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Tumaini, Zainabu Mtinda, alisema mafanikio ya shule hiyo ambayo ni ya serikali yametokana na ushirikiano mzuri wanaoupata kutoka kwa wananchi wa Kata ya Kinampanda, serikali ya wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla. Mtinda alisema malengo ya shule hiyo ni kuhakikisha inakuwa miongoni mwa kumi bora kitaifa ambayo yatatimia kutokana na ushirikiano mkubwa wanaoupata.

Mkuu huyo wa shule aliiomba serikali kuwasaidia kujenga uzio wa shule ili kuimarisha ulinzi na usalama kwa wanafunzi.

# H'shauri yajitolea kujenga kituo cha kisasa cha afya

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro kwa mara ya kwanza tangu ilipoanzishwa imeamua kufanya ujenzi wa mradi mkubwa wa kituo cha kisasa cha afya katika Kata ya Tungi ambacho kitagharimu Sh. bilioni 1.2 zinazotokana na mapato ya ndani.

Akizungumza katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani, Meya wa Manispaa hiyo, Pascal Kihanga, alisema tayari ujenzi wa majengo 10 ya kituo hicho umeanza ambayo yanakakadiriwa kutumia Sh. milioni 350.

"Leo nafurahi kuwaambia kuwa tangu manispaa ianzishwe miongo kadhaa iliyopita, haijawahi kujenga kituo cha afya yenyewe kwa mapato yake ya ndani, leo manispaa hii chini ya baraza hili inajenga kituo cha afya cha Tungi ili kuwasogezea huduma wananchi," alisema Meya Kihanga.

Alisema pamoja na kujenga kituo hicho katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022, manispaa ilitumia Sh. milioni 424.5 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa zahanati tisa.

Kihanga alisema kati ya zahanati hizo, sita zimakamilika na zinatoa huduma kwa wananchi kwenye kata za Tungi, Kihonda Maghorofani, Mbuyuni, Mgaza-Mindu, Sultan Area na Kiwanja cha Ndege, wakati zahanati tatu zipo kwenye hatua mbalimbali za umaliziaji.

"Hivi vitu havijawahi kufanyika katika kipindi cha miaka ya nyuma, ukiangalia nyuma na sasa ni tofauti sana, bado niendelee kulipongeza Baraza la Madiwani na wataalamu kwa kazi nzuri mnayoifanya," alisema Kihanga.

Meya huyo alisema kuwa manispaa inakwenda kubadilika na katika mabaraza yaliyopita hayajawahi hata kwa wakati mmoja kujenga zahanati mbili kwa wakati mmoja.

"Leo tunazungumzia zahanati tisa, sita zikikamilika na tatu zipo kwenye umaliziaji," alisema Kihanga.

Alisema endapo baraza hilo kwa kushirikiana na wataalamu likiendelea na mwenendo wa kusimamia huduma za kijamii, upo uhakika baada ya muda mfupi kata zote zilizopo katika manispaa hiyo zitakuwa na zahanati za kisasa.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Morogoro mjini, Slyvester Yaredi, alisema ni nadra kukuta halmashauri ya manispaa ikajenga kituo cha afya.

Alisema, aliwahi kutembelea eneo la ujenzi wa kituo hicho cha afya eneo la Tungi ambacho kikikamilika kwenye ukanda huo wananchi watakuwa na nafasi kubwa ya kupata huduma za afya.

Katibu wa CCM wilaya hiyo pia alipongeza hatua ya manispaa hiyo kwa kujenga zahanati tisa ambazo kati ya hizo, sita zinafanya kazi kwa kutoa huduma.

Yaredi alisema anatarajia kuona malengo yaliyopo kwa manispaa hiyo kuwa kabla ya kufika mwaka 2025, maboma zahanati ambazo zimekaa zaidi ya miaka 18 bila kukamilishwa zinapaswa zikamilishwe ili zitoe huduma za afya kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela alisema uamuzi wa kujenga zahanati hizo tisa huku sita zikiwa zimekamilika kwa kutumia fedha za mapato ya ndani, serikali kuu umewaletea watumishi 18 wakiwamo madaktari na wauguzi. "Endapo tutaendelea na kuanzisha juhudi zetu binafsi kwa mapato yetu ya ndani ikiwamo kujenga zahanati ndivyo nayo serikali kuu itakavyoongeza nguvu na kutupatia watumishi wa afya kwani licha ya hao, imetupatia wengine saba kwenye hospitali yetu ya wilaya wakiwamo madaktari wawili na wauguzi watano," alisema Machela.



Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, aliposwasili katika ufunguzi wa semina maalum iliyoandaliwa na Benki ya CRDB kwa ajili ya taasisi, mashirika, na wakala za serikali iliyofanyika katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam. Wengine pichani ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa benki hiyo, Bruce Mwile, Mkurugenzi wa Mawasiliano CRDB, Tully Mwambapa na Ofisa Mkuu wa Fedha, Fredrick Nshekanabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DMI yapigia debe mafunzo ya uhandisi, uendeshaji meli

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kimewataka Watanzania kuchangamkia fani za unahodha wa meli na uhandisi ambazo wanafunzi wanaodahiliwa wanapata mikopo chuoni hapo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Udahili wa chuo hicho, Lusajo Martini wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu chuo hicho kwenye maonyesho ya vyuo vikuu nchini.

Alisema fani za bahari kwa ujumla ikiwamo ya uhabaria, uhandisi na uendeshaji wa meli zina soko kubwa duniani na wahitimu wote wanaomaliza chuo hicho wamekuwa wakiajiriwa kwenye kampuni za ndani na nje ya nchi. Alisema DMI ina Mfuko wa Mafunzo unaoita METFUND Education Training Fund, ambao umekuwa ukitoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma fani ya uhandisi na uendeshaji wa meli kama sehemu ya kuhamasisha watu wengi kujiunga na fani hizo.

Pia alisema ndani ya DMI kuna wakala iitwayo Manning Agency ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiwaunganisha wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo na kampuni mbalimbali za meli duniani kwa ajili ya ajira.

"Hizi fani ajira zake siyo za kutafuta ziko nyingi sana, mwanafunzi anapohitimu wakala anawaunganisha na kampuni mbalimbali za meli na za usafirishaji zinazotafuta wafanyakazi kwa hiyo niwahakikishie watakaokuja kusoma DMI kwamba hawatahangaika kutafuta ajira," alisema.

Alisema DMI ni chuo pekee nchini kinachotoa mafunzo yanayohusiana na uendeshaji wa meli na uhandisi kwenye meli na mafunzo yake yamepata ithibati ya kimataifa.

"Kwenye meli ukiachana na shughuli zile zinazofanyika baharini kuna shughuli za nchi kavu za uratibu wa masuala ya bahari na hao pia tunawapa mafunzo pia ya usafirishaji tunawaomba wachangamkie dirisha la udahili limefunguliwa wanafunzi wafanye udahili kwa njia ya mtandao," alisema.

Martini alisema Afrika nzima vyuo vinavyotoa mafunzo yanayofanana na DMI viko vinne tu na mafunzo wanayotoa hayana ushindani hapa nchini kutokana na kuwa ndiyo taasisi pekee inayotoa mafunzo ya aina hiyo.

Alisema DMI imepata usajili kutoka kwa Taasisi ya Kimataifa ya International Maritime Organization (IMO), kutoa mafunzo ya bahari na wahitimu wa chuo hicho wanaweza kufanyakazi popote pale duniani.

Alisema wanafunzi wote walioomaliza kidato cha sita au waliosoma ngazi ya astashahada wanaweza kujiunga na chuo hicho kwenye fani mbalimbali kwa mwaka wa masomo ulioanza.

Alisema pia DMI inatoa mafunzo ya awali kabisa ya namna mtu anavyoweza kujiokoa yanapotokea majanga kwenye bahari.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa ajili ya kujihami kwani mtu anayepata mafunzo hayo anaweza kuokoa maisha yake na ya wengine pindi kunapotokea janga lolote baharini.

# CBE kuendeleza wanafunzi mawazo kibiashara

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeanzisha programu atamizi ambayo inatumika kuendeleza mawazo ya biashara yanayotolewa na wanafunzi wanaosoma kwenye chuo hicho kuwa bidhaa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Programu za Uanagenzi chuoni hapo, Dk. Mariam Tambwe, wakati akizungumza kwenye maonyesho ya vyuo vikuu yaliyomalizika hivi karibuni.

Alisema programu hiyo inalenga kuwawezesha wanafunzi wa chuo hicho kuwa mahiri na kuanzisha biashara zao wanapomaliza masomo yao badala ya kutembea na vyeti wakihangaika kutafuta ajira.

Dk. Mariam alisema wanawafundisha wanafunzi kuja na mawazo ya biashara ambayo chuo kinayachuja na baadaye kuwaongoza namna ya kuyatekeleza mawazo hayo kwenda kwenye uhalisia kwa kutengeneza bidhaa au kuanzisha biashara huku wakiendelea na masomo yao.

"Hii programu ni nzuri sana kwasababu mwanafunzi anafundishwa biashara kwa kutumia wazo alilolitoa na akimaliza shule wazo lake la biashara linakuwa limeshakuwa bidhaa, sasa badala ya kuhangaika kutafuta ajira anajiajiri mwenyewe na kuajiri vijana wenzake," alisema.

Alisema programu atamizi sio kozi maalum bali ni kwa mwanafunzi yeyote anayesoma CBE masomo yoyote kwa kuwasilisha wazo lake la biashara na mpaka sasa wameshapokea mawazo 32 ya biashara ambayo wanaendelea na mchakato wa kuyachuja mpaka wapate watakayoyaendeleza.

Alisema matarajio ya chuo hicho ni programu hiyo kuwanufaisha wanafunzi zaidi ya 500 kwa mwaka na watashirikiana na wakufunzi mbalimbali wa vyuo na wajasiriamali kwa ajili ya kuwafundisha.

Kuhusu programu ya uanagenzi, Dk. Mariam alisema itamwezesha mwanafunzi kusoma mafunzo yake nusu chuoni na nusu kwa mwajiri na itaanza mwaka 2023 na nia ni kumwezesha mwanafunzi kupata na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira.

Alisema hivi sasa wako kwenye mchakato wa kuandaa mitaala ya programu hizo na wataanza kwa tatu za uanagezi katika teknolojia ya digitali, mizani na viwango, benki na usimamizi wa mikopo.

"Tumeanza na kozi chache kwasababu ndiyo tunaanza kwa majaribio, lakini kwasababu ya mahitaji ya soko tutaongeza kozi zingine kadri mahitaji yatakavyoongezeka kwa sasa tutaanza na kozi hizi tatu," alisema.

Alisema CBE iliamua kuanzisha kozi hizo baada ya waajiri wengi kulalamika vyuo vinazalisha wahitimu ambao hawajaiva vya kutosha hivyo kulazimika kuwapa mafunzo ya muda mrefu wanapowaajiri kwenye kampuni zao.

Alisema malalamiko kama hayo yanatolewa na waajiri sio Tanzania pekee bali dunia nzima, wahitimu wengi kwa sasa hawakidhi mahitaji ya soko la ajira kutokana na kukosa umahiri wa hali ya juu kwenye fani mbalimbali wanazosomea.

"Wanalalamika kwamba wahitimu wengi wanaozalishwa vyuoni ni tofauti na mahitaji ya soko ndiyo sababu CBE sasa tumeamua kuja jibu la changamoto hiyo kwa kuanzisha program ya uanagenzi ambapo mwanafunzi atasoma nusu darasani na nusu kwa mwajiri," alisema.

# Mbunge kulipa posho walimu wanaojitolea

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Jimbo la Songwe, Philip Mulugo, ameahidi kutoa Sh. 330,000 kila mwezi kwa ajili ya kuwalipa mshahara walimu 11 wanaojitolea katika Shule ya Sekondari ya Namalaji, Kata ya Totowe wilayani humo.

Aidha, Mulugo aliahidi kutoa shilingi milioni tatu mwezi Novemba, mwaka huu, kwa ajili ya kununulia mashine ya kudurufu (photocopy machine) ambayo itasaidia walimu wakati wa mitihani ya wanafunzi.

Mulugo alifikia uamuzi huo baada ya kutembelea shule hiyo iliyoanzishwa Januari 17, mwaka huu na kuelezwa kuwa shule hiyo ina walimu watatu walioajiriwa na serikali, lakini 11 wanafundisha kwa kujitolea.

Wanafunzi hao walimweleza mbunge huyo kuwa walimu hao wanaojitolea wanalipwa kupitia michango ya wazazi ya Sh. 6,000, na baadhi hawatoi fedha hizo hali inayosababisha walimu wao kupata shida.

Kutokana na hali hiyo, Mulugo aliahidi kuanza kutoa Sh. 330,000 kila mwezi kulipa posho za walimu hao wakati wanasubiri ajira za serikali na zitatumwa kwa Diwani wa Kata ya Totowe ambaye ataziwasilisha kwa mkuu wa shule hiyo.



Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Octavian Mshiu, akimwelekeza jambo Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Goodluck Mbanga (kulia), wakati wajumbe wa bodi hiyo wakikagua machimbo ya mawe ya kujengea barabara yaliyoko Nyashada jijini Mwanza. **PICHA: THERESIA MWAMI**

# Vijiji 19 kupatiwa huduma ya maji

**Na Restuta Damiana,** BUKOBA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoani Kagera unaendelea kutekeleza miradi ya maji kwenye vijiji 19 vyenye wanufaiaka 127,827 kwa bajeti ya mwaka 2022/2023 ili kufikisha huduma kwa wananchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Mhandisi Patrice Jerome, wakati akitoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa huduma hiyo kwa mwaka 2021/2022 na miradi inayoendelea kutekelezwa 2022/2023.

Jerome alisema, katika kuongeza kasi ya utendaji na kufikia lengo la serikali kama sehemu ya mpango wa maendeleo kwa wananchi mkoa umefanya na kufikia asilimia 70 ya upatikanaji wa majisafi vijijini.

Aidha, alisema licha ya kuwa na tatizo la miradi kuendelea kutekelezwa zaidi ya mwaka mmoja kutokana na sababu mbalimbali, wakala unaongeza jitihada kwa kila wilaya ili kufikia maeneo yote yanayokaliwa na wananchi.

"Kuna tatizo la miradi ya kutekelezwa zaidi ya mwaka mmoja kulingana na gharama kuwa kubwa kuliko uhalisia wa bajeti iliyopangwa mfano miradi ya fedha za maendeleo ya ustawi wa jamii, inakuwa na upungufu wa kutosheleza maeneo ya utekelezaji ndani ya wilaya," alisema Jerome.

Alisema kwa mwaka 2021/2022 kulikuwa na miradi 33 inayotekelezwa kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha na saba miradi ya maendeleo ya ustawi wa jamii UVIKO kwenye vituo 105.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka 2021/2022 RUWASA iliidhinishishiwa gharama ya Sh. bilioni 22.1 kutoka Mfuko wa Maji wa Taifa (NWIF), lipa kwa matokeo (PbR) programu ya matokeo (PfrR), fedha ya mfuko wa maendeleo na ustawi wa jamii (UVIKO-19) na ruzuku (GOT).

"Kwa vyanzo vyote kunakuwa na kiasi kilichotengwa ambacho ni milioni 25.3, lakini hadi mwezi Juni mwaka huu kiasi kilipokelewa ni bilioni 24.5," alisema Jerome.

Mhandisi wilayani Kyerwa, Shukrani Tungaraza alisema, mbali na usimamizi wa miradi zipo jitihada kuhakikisha wanapata huduma za maji hadi majumbani.

"Sio tu kuweka miradi tunatoa vipaumbele kwa watumia maji ambao ni wananchi kufikisha kwenye majumba yao kwa kufunga bomba na wao kulipia ankra," alisema Tingaraza.

Alisema, njia hiyo ya maji itasaidia wakusanyaji wa fedha za ankra ya maji zitakazo hudumia ukarabati wa miundombinu inayochakaa au kuharibika.

Awali, akifungua kikao hicho Mkuu wa Mkoa wa Kagera Meja Jenerali Charles Mbuge alisema, serikali ina mpango wa kuona miradi inakuwa endelevu na imara kumnufaisha mwananchi.

Aliongeza kuwa, mbali na kuwapo muda mwingi ukamilishaji wa miradi, baadhi ya matatizo yameweza kutatuliwa na wizara kwa kutoa usafiri wa pikipiki 12 kwa mkoa huo ikiwa ni kufikia maeneo.

Nipashe
Spotika



WATANO WANAOTAKIWA KUTHIBITISHA UBORA EPL UK. 12-13



# HADITHI YA LEWANDOWSKI NA BAYERN

**BARCELONA,** Hispania

HATIMAYE imetokea. Baada ya miezi kadhaa ya uvumi, Robert Lewandowski amejiunga na Barcelona.

Hatua hiyo imeashiria mwisho wa uhusiano wa miaka nane kati ya Lewandowski na Bayern Munich ambao uliwafanya kushinda ubingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, mara nane mfululizo na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2020.

Hata hivyo, mambo hayakuisha kwa maelewano mazuri. Lewandowski ameelezea mara kwa mara kufadhaika kwake kuhusu mwajiri wake wa muda mrefu katika wiki za hivi karibuni.

Alipolazimishwa kurejea kwenye mazoezi ya timu katika wiki ya tatu ya Julai, alifika kwa hasira kwa siku tatu mfululizo na alionekana kuwa mvivu wakati wa mazoezi.

Ikiwa mshambuliaji huyo alikuwa mkweli aliposema muda mfupi uliopita kwamba "sioni uwezekano wowote wa kuichezea klabu hii tena." Wengi karibu na Bayern waliona kama mbinu ya kulazimisha kuondoka kwenye mkataba wake.

Lakini, kama msemo unavyokwenda, sio muhimu kile ambacho watu hufikiria unapokuja kama vile wanavyofikiria unapoondoka.

Matukio ya wiki za hivi karibuni yanaweza kuharibu urithi wa Lewandowski katika klabu ya Bayern - zaidi kwa sababu ni mara ya pili katika maisha yake ya soka kulazimisha kuhama kabla ya kumalizika kwa mkataba wake, kwani alifanya kitu kama hicho mwaka 2013 alipokuwa na Borussia Dortmund. .

**HISTORIA MPYA?**

Ikiwa tutajaribu kuelewa hisia za Lewandowski, kunaweza kuwa na sababu za msingi za yeye kushinikiza kuhamia Barcelona msimu huu wa joto. Licha ya rekodi nzuri ya mabao 344 katika mechi 375 katika kipindi hiki cha miaka nane akiwa Bayern, Lewandowski alilazimika kusubiri kwa muda mrefu kabla ya kutambuliwa kimataifa.

Amesikitishwa sana na ukweli kwamba wapigakura wa Ballon d'Or wamempuuza mara kwa mara. Lewandowski ameshinda tu tuzo ya Mchezaji Bora wa Wanaume wa Fifa mwaka 2020 na 2021.

Kwa ujumla zaidi, Lewandowski hajajenga aina ya thamani ya jina unayoweza kutarajia kutoka kwa mmoja wa washambuliaji mahiri wa kizazi chake. Mikataba ya udhamini wa fedha nyingi imeenda kwa wachezaji wengine.

Hivi karibuni atafikisha miaka 34, sasa inaweza kuwa nafasi ya mwisho ya Lewandowski kufaidika na uchezaji wake kibiashara na kuacha historia kubwa zaidi. Timu iliyofufuliwa ya Barcelona chini ya Kocha Xavi Hernandez inaweza kuwa mahali pazuri pa kufanya hivyo. Lewandowski atakuwa mshambuliaji chaguo la kwanza pale Camp Nou, kama alivyokuwa Bayern kwa miaka nane.

**MSHAMBULIAJI BORA**

Wakati Bayern ilipomsajili Lewandowski mwaka 2014, na kumvuta mbali na wapinzani wao Dortmund, hawakujua kama Lewandowski angekuwa mfungaji mabao wa kutegemewa na sasa watu wamejenga hoja kwamba, raia huyo wa Poland ndiye mshambuliaji bora zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Uthabiti wa Lewandowski, pamoja na mtazamo wake wa kitaaluma na orodha ndogo ya majeruhi, vilimfanya awe wa kuaminika sana. Kwa wastani, Lewandowski aliichezea Bayern mechi 47 kwa msimu.

Zaidi ya hayo, uwezo mwingi wa Lewandowski ulimruhusu kuzoea makocha wapya kwa urahisi. Alifanya kazi sawa chini ya Pep Guardiola, Carlo Ancelotti, Hansi Flick na Julian Nagelsmann. Wakati baadhi ya wachezaji wenzake waliwalazimisha makocha wa Bayern kufanya marekebisho ya kimbinu, hawakuwahi kuwa na wasiwasi kuhusu Lewandowski - wala hawakuwa na wasiwasi kuhusu kelele zozote za kukatisha tamaa.

Kando na vita vya kisheria na wakala wake wa zamani na mshirika wa kibiashara, Cezary Kucharski, Lewandowski hakuwahi kutangaza habari hiyo na kitu kingine chochote isipokuwa kiwango uwanjani.

**SI KIPENZI CHA MASHABIKI**

Uhusiano kati ya Lewandowski na Bayern ulikuwa wa upande mmoja. Katika kipindi cha miaka nane iliyopita, alibadilika kutoka mshambuliaji wa mpito mwenye nguvu nyingi hadi namba tisa mwenye kujali zaidi ambaye amejifunza kuelewa uchezaji wa nafasi na kutumia mwendo mzuri wa nje ya mpira, huku pia akiboresha ujuzi wake wa kiufundi katika nafasi yake.

Kwa maana fulani, aligeuka kuwa mshambuliaji kama roboti anayelingana na tabia yake ya jumla. Mashabiki hawakuwahi kumchukua mfungaji wao kwenye mioyo yao licha ya mchango wake katika mafanikio ya Bayern.

Lewandowski mwenyewe pia hakuwahi kuficha ukweli kwamba fedha zilikuwa dereva wake mkuu. Alipoongeza mkataba wake mwaka wa 2019, alisema kuwa Bayern ndiyo klabu sahihi kwake wakati huo. Hakukuwa na kiapo cha utii wa milele.

Kwa kuzingatia hilo, kuondoka hivi majuzi kutoka Munich hakukutarajiwa kabisa. Baada ya yote, inaweza isiharibu sana urithi wa Lewandowski kwa sababu hakukusudiwa kuwa kipenzi cha mashabiki.

Badala yake, Lewandowski daima ataonekana kama mfanyabiashara anayetafuta kazi yake mwenyewe.

## ISIKUPITE

KLABU ya Al Ahly ya nchini Misri imethibitisha kuwa winga wake, Luis Miquissone amepona kabisa jeraha lake la goti na yuko fiti kwa michezo ijayo. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Msumbiji, alisajiliwa na Ahly kutoka timu ya Simba.



Extra Time

# WATANO WANAOTAKIWA KUTHIBITISHA UBORA EPL

**LONDON,** England

MSIMU mpya wa Ligi Kuu England unakaribia na nyota wachache wana sababu nyingi zaidi ya kuvutia.

Iwe ni kurejesha sifa zao, kuwathibitishia wenye shaka kuwa wamekosea au kuhalalisha mauzo yao ya bei kubwa, wataona msimu huu unakuja kama fursa ya kurekebisha baadhi ya makosa.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wanatakiwa kuthibitisha ubora wao kwenye Ligi Kuu wakati wa msimu huu 2022-2023.

**#1 .Jack Grealish (Manchester City)**

Ingawa kushinda Ligi Kuu ya England katika msimu wake wa kwanza hakuwezi kuonekana kama kushindwa, Jack Grealish atajua kuna mengi yanatakiwa kutoka kwake akiwa Manchester City.

Fowadi huyo wa England alikuwa mchezaji ghali zaidi wa nchi hiyo wakati City ilipotoa pauni milioni 100 kumsajili kutoka Aston Villa majira ya joto yaliyopita.

Akiwa na bei kama hiyo, rekodi yake ya kufunga mabao matatu na kutoa pasi tatu za mabao kwenye ligi msimu uliopita ni ya kuridhisha kwa kiasi fulani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alianza mechi 22 tu kati ya 38 za kikosi chake kwenye Ligi Kuu na hata aliachwa kwenye benchi na Pep Guardiola kwenye pambano la City la kuamua taji la Ligi na klabu yake utotoni ya Villa siku ya mwisho.

Kulikuwa na mwanga mwingi wa kile mshambuliaji mahiri anaweza kutoa, na Grealish atajihisi yuko tayari kujifanya kuwa mtu muhimu kwa mabingwa hao muhula huu.

**#12. Gabriel Jesus (Arsenal)**

Baada ya kukaa kule Manchester City, Gabriel Jesus ana nafasi ya kuwa nyota baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 45 kwenda Arsenal.

Mshindi huyo mara nne wa Ligi Kuu ya England amepuuza mapendekezo ambayo yalikuwa ni motisha nyuma yake.

Alisema: "Sitaki kuwa mtu mkuu hapa, sitaki kuwa nyota.

"Nataka kucheza na kufurahia soka, ndicho ninachopenda kufanya. Nilikuja kuwasaidia vijana. Ni wachezaji wa ajabu pia. Ni klabu ambayo kila mtu anataka kushinda pamoja."

Lakini kitendo cha Pep Guardiola kutomtumia mara kwa mara mchezaji huyo wa zamani wa Palmeiras pale City kuliacha swali la kufaa kwake kama namba 9 wa timu, licha ya kipaji chake kuonekana wazi.

Akiwa na rekodi ya kufunga mabao 58 katika mechi 159 za Ligi Kuu ya England, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuhisi kuwa hiyo si tathmini ya haki na atataka kuondoa shaka yoyote kwa kufanya makubwa pale Emirates.

**#13. Marcus Rashford (Manchester United)**

Inasikitisha kuona jinsi hisa za Marcus Rashford zimeshuka katika miezi 12 iliyopita.

Baada ya kukosa penalti wakati wa kichapo cha kuhuzunisha cha England kwenye fainali ya Euro 2020 kutoka kwa Italia msimu uliopita wa joto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alikosa kuanza kwenye kampeni ya klabu mpya ya Manchester United baada ya kuhitaji kufanyiwa upasuaji kutokana na jeraha la bega.

Baadaye alitatizika kufikia kiwango cha juu katika msimu uliokumbwa na matatizo kwa ujumla kwa Mashetani Wekundu, akifunga mabao matano pekee katika mechi 32 katika michuano yote na kupoteza nafasi yake kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Kwa kuwa michuano ya Kombe la Dunia inakaribia, hilo ni jambo ambalo atataka kubadilika haraka.

Rashford alisema wiki iliyopita kuhusu kampeni hiyo mpya: "Ni fursa ya kujiburudisha. Niko tayari kwenda tena.

"Tunaweza kufanya mengi pamoja. Kwangu mimi ni mwanzo mpya, kitu ambacho ninatazamia."

**#4. Aleksandar Mitrovic (Fulham)**

Baada ya kuvunja rekodi ya mabao 43 kwenye michuano yote kwa Fulham msimu uliopita, inaweza kuonekana kuwa ya ajabu kupendekeza Aleksandar Mitrovic ana uhakika wa kuthibitisha ubora wake tena.

Lakini sababu ya mikondo ya awali ya Mserbia huyo na kuna sababu ya kupendekeza atakuwa mwanamume kwenye misheni akirejea hivi punde.

Alifanikiwa kufunga mabao matatu pekee ya ligi msimu wa 2020-2021, akianza mechi 13 pekee huku kukiwa na ripoti za kutofautiana na kocha wa wakati huo, Scott Parker.

Na huku Mitrovic akiwa amesimamia zaidi ya mabao 10 katika kampeni zake nne zilizopita za Ligi Kuu, bado kuna dhana kwamba hawezi kuzalisha katika kiwango cha juu.

Akitoka nyuma ya msimu wa mafanikio zaidi wa kazi yake, atahisi kuwa tayari kuweka kiwango chake cha juu zaidi.

**#5 Dele Alli (Everton)**

Dele Alli anaonekana kukosa nafasi za kujenga upya heshima yake kwenye Ligi Kuu England.

Wakati wa misimu mitatu ya kwanza ya mhitimu huyo wa akademi ya MK Dons kule Tottenham Hotspur, alionekana kuwa mmoja wa vipaji angavu zaidi vya England.

Lakini katika kipindi cha miaka minne iliyopita, kukosekana kwa maendeleo kwa kiungo huyo kumekuwa mbaya na kumfanya Januari apelekwe Everton na ndiko kidogo kukamboresha.

Mambo yanaweza kubadilika haraka katika soka ingawa Everton imenusurika kushuka daraja chini ya Frank Lampard msimu uliopita, Alli anaweza kuuona msimu huu kama fursa ya mwisho ya kufufua soka lake.


Kurejeshwa kwenye timu ya kimataifa inaonekana nje ya swali hivi sasa, lakini mwanzo mzuri wa kampeni unaweza kumrudisha kwenye mazungumzo mbele ya kuelekea Qatar kwenye Kombe la Dunia.



GABRIEL JESUS

## Nukuu

"WATU wakati mwingine husema kuna ushindani kati yangu na Mohamed Salah, lakini unajua sijioni kuwa na ushindani na mchezaji yeyote. Tuna uhusiano mzuri, tunatumiana ujumbe kila mara. Nadhani vyombo vya habari kila wakati vinajaribu (kuongeza) mambo." **Sadio Mane**



"SINA uhakika kama ninaweza kumpa Cesar Azpilicueta Azpi kile anachotaka. Wakati fulani ni kuhusu kile tunachotaka. Nililinganisha tu ni kiasi gani tulipigania kwa (Kalidou) Koulibaly, napata tabu." **Thomas Tuchel**




"Tuna furaha sana Oleksandr Zinchenko Alex amejiunga nasi. Ni mchezaji ambaye binafsi namfahamu vizuri na niliendelea kumfuatilia baada ya muda wangu Manchester City. Ni mchezaji wa ubora wa juu ambaye atatupa chaguzi na uwezo mkubwa," **Mikel Arteta**





Yassin Mustapha, mmoja wa wachezaji waliozihama klabu zao kwenye Ligi Kuu kwenda kujiunga na klabu zingine. Hapa akiwa kwenye klabu yake ya zamani ya Yanga kwenye moja kati ya mechi za Ligi Kuu msimu uliopita. Msimu huu amejiunga na Singida Big Stars.

# WACHEZAJI WANAVYOPISHANA USAJILI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HUYU katoka huku kaenda huku na huyu kaondoka huku, katua kule, ndivyo unavyoweza kusema kwenye usajili unaoendelea kushika kasi kwa sasa kwa klabu za Ligi Kuu.

Kumekuwa na mpishano wa wachezaji wanaotoka klabu moja kwenda nyingine, na wa huku nao wanakwenda kwingine, ili mradi tu kila klabu inaona kuwa mchezaji fulani atatufaa kwa msimu ujao wa mashindano.

Kwa sasa klabu zimekuwa kwenye harakati za kutengeneza vikosi vyao ili kukabiliana na mshindano mbalimbali, ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23, ambayo wengi wanatarajia itakuwa ni ngumu na ya kusisimua.

Zipo klabu ambazo zimekuwa zikiachana na wachezaji wao wengi na papo hapo kusajili wachezaji wengine ambao wanaona watafaa.

Klabu za KMC, Kagera Sugar, Dodoma Jiji na Polisi Tanzania zinaonekana kuacha wachezaji wengi sana. Wengine wamechukuliwa na klabu zingine, baadhi wamemaliza mikataba na wengine hawana mpango wa kuendelea nao.

Kwenye makala haya tutazitizama klabu ambazo kwa sasa hazishikiki kwenye usajili zimekuwa zikisajili wachezaji.

Wachezaji tutaowaweka hapa ni wa hapa hapa nchini, wanaliosajiliwa kutoka klabu moja ya Tanzania na kwenda nyingine, haijalishi kuwa ni wa Kitanzania au wakigeni.

Na usajili tutaouzungumza hapa ni ule ambao umeshakamilika.

**1. Dodoma Jiji**

Klabu ya Dodoma Jiji ndiyo inayoonekana kuongoza mpaka sasa kwenye kinyang'anyiro cha usajili mpaka sasa.

Imewasajili wachezaji Christian Zigah raia wa Ghana, Mkenya Collins Opare na kipa Daniel Mgore, wote kutoka Biashara United ambayo kwa sasa imeshuka daraja, msimu ujao itacheza Championship, Amani Kyata na Rashid Chambo, hawa wametoka Coastal Union, Hassan Mwaterema kutoka Kagera Sugar, Jimmy Shoji kutoka Mbeya Kwanza na Salum Kihimbwa akitokea Mtibwa Sugar.

**2. Singida Big Stars**

Ni timu ambayo itacheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/23 baada ya kupanda Ligi Kuu. Ilipanda kwa kutumia jina la DTB, lakini baada ya kumalizika kwa Ligi ya Championship, ikabadili jina na kujiita Singida Big Stars.

Nayo inafukuzana na Dodoma Jiji kwa kusajili wachezaji wengi mpaka sasa.

Imemnasa kipa Metacha Mnata kutoka Polisi Tanzania, Abdumajid Mangalo aliyekuwa timu ya Biashara United, Kelvin Sabato na Said Ndemla kutoka Mtibwa Sugar, Paul Geofrey na Yassin Mustapha kutoka Yanga.

**3. Ihefu FC**

Hawa ndiyo Mabingwa wa Ligi ya Championship, timu iliyocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu wa 2019/20, ikashuka daraja msimu huo huo, lakini ikacheza tena ligi ya chini kwa msimu mmoja kabla ya kurejea tena Ligi Kuu.

Jana nayo ilitangaza wachezaji wanne wazoefu ambao imewasajili kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.

Nao ni Peter Mwalyanzi na Mwaita Gereza kutoka Kagera Sugar, Obrey Chirwa kutoka Namungo FC, Jaffar Kibaya kutoka Mtibwa Sugar , Juma Nyosso aliyekuwa Geita Gold.

**4. Simba SC**

Klabu ya Simba msimu huu imeamua kusajili wachezaji wawili tu kutoka kwenye klabu za humu nchini.

Wachezaji waliopata bahati ya kusajili wa klabu hiyo ni Nassor Kapama kutoka Kagera Sugar na Habib Kyombo kutoka Mbeya Kwanza.

**5. Azam FC**

Pamoja na kusajili wachezaji mbalimbali kutoka nje, hawajasahau kusajili wachezaji wa ndani.

Nao kama Simba wamesajili wawili tu mpaka sasa. Wachezaji hao ni Abdul Selemani 'Sopu' kutoka Coastal Union na Cleophace Mkandala aliyetokea Dodoma Jiji.

**6. Kagera Sugar**

Kagera Sugar ni moja ya timu iliyoondokewa na wachezaji wengi msimu huu. Ni zaidi ya 10, lakini mpaka sasa yenyewe imefanikiwa kusajili mchezaji mmoja tu mpaka sasa ambaye ni Datius Peter ambaye ametokea Polisi Tanzania.

## JE, WAJUA?



ILI kukabiliana na tishio la ugaidi, waandaaji wa Kombe la Dunia nchini Qatar wametangaza kutumia ndege zisizohitaji rubani 'Drones' ili kudhibiti usalama wa viwanja. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Qatar imeingia makubaliano na kampuni ya Fortem Technologies ambayo itatoa ndege hizo ili kuongeza ulinzi kwenye mashindano hayo.



# Vikundi 400 vyaunganishwa kupata mikopo

**Na Peter Mkwavila,**

CHAMWINO

VIKUNDI 400 vya wafugaji na wakulima katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa mkoani Dodoma, vimeunganishwa na kusajiliwa ili kupata mikopo nafuu kwa taasisi za fedha.

Mkurugenzi Mkuu wa Dodoma Halisi Limited Tanzania, Anthony Msanga, aliyasema hayo jana katika kikao cha wadau wa maziwa sambamba na uzinduzi wa kampeni ya ufugaji ng'ombe wa kisasa wa maziwa wilayani Chamwino.

Alisema kampuni hiyo imefanikisha kuwaunganisha ili kupata fursa ya mikopo na elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa.

"Elimu hiyo ya ufugaji bora ya ng'ombe wa maziwa ikiwamo na kitendo cha kuwaunganisha kwa pamoja, ni imani yetu wataweza sasa kupata fursa za mikopo nafuu kwa urahisi na hatimaye lengo letu la kuamsha ufungaji bora wenye tija kibiashara watafanikiwa kutimiza ndoto zao," alisema.

Hata hivyo, alisema kampuni imejipanga kuhakikisha wafugaji wanafuga kisasa na kuwa na uhakika wa malisho na maji.

Alisema elimu inayotolewa ni pamoja na namna ya kuaandaa na kuhifadhi malisho ya mifugo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, aliwataka wafugaji kuhakikisha wanatumia fursa ya ufugaji bora na wenye tija kupitia vikundi hivyo.

"Niwasihi wafugaji ni wakati sasa wa kuachana na ufugaji wa kizamani, tumieni fursa ya kufuga mifugo michache ili kupata faida atakayoweza kuwamudu katika kuwahudumia," alisema.

Aidha, alizitaka pia taasisi na kampuni zingine kutoa fursa ambazo zinazowagusa jamii na zinazowainua kiuchumi.



Mkurugenzi Mkuu wa Dodoma Halisi Limited, Antony Msanga, akizungumza na wadau wa maziwa wa Mkoa wa Dodoma kwenye uzinduzi wa kampeni ya ufugaji ng'ombe wa maziwa wa kisasa uliofanyika Chamwino jana, wengine waliokaa (wa tatu kushoto) Mwenyekiti wa Maaridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Evance Chande na (wa pili kulia) Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC atoa siku 10 h'shauri kupitia taarifa za usambazaji dawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ametoa siku 10 kwa wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kukutana na kupitia taarifa za upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa kwenye maeneo yao.

Vile vile, amewataka kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi ambao watabainika kuhusika na upotevu au upungufu wa dawa katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mkoa.

Mtaka alibainisha hayo jijini hapo katika kikao chake na viongozi wa wilaya katika sekta ya afya, kwa ajili ya kupitia taarifa ya upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa.

"Hizi siku 10 tunazopeana ziwe za kazi ambazo lengo lake ni kufanya ukaguzi na kujiridhisha kwa dhati kuhusu matokeo ya dawa kwenye vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na mkoa. Baada ya hapo kutakuwa na kikao cha kupokea taarifa na kutapobainika upungufu wakurugenzi wanayo nafasi ya kuchukua hatua za kinidhamu."

"Tutakaa kikao kingine cha kupokea taarifa ya ukaguzi wa vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na mkoa kwa asilimia 100 katika upokeaji, utoaji na usambazaji wa dawa na baada ya hapo katibu tawala wa mkoa ataweza kuchukua hatua kwenye maeneo ambayo yameonyesha upungufu," alisema.

Kadhalika, alisema taarifa itakayotolewa na wakurugenzi ionyeshe dawa kiasi gani zimepokelewa, thamani ya dawa, thamani ya upungufu na upotevu ili kulinganisha waliyopokea kutoka serikali kuu na wadau wengine.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, alisema kikao hicho ni muhimu kutokana na serikali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha huduma za afya.

Alisema maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wameyachukua na wanaenda kuyafanyia kazi na kuhakikisha siku 10 alizotoa wanapitia taarifa na kuchukua hatua kama walivyoagizwa.

"Kikao kimeenda vizuri na sisi tukiwa kama wasimamizi wakuu wa fedha katika ngazi ya wilaya tutahakikisha tunapitia taarifa kama tulivyoagizwa na pale ambapo tutaona kuna haja ya kuchukua hatua hatutasita kufanya hivyo," alisisitiza Dk. Nkullo.

# Watakiwa kujiepusha rushwa uvalishaji hereni mifugo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wataalamu wa mifugo kuepuka kuomba rushwa kwa wafugaji katika uvalishwaji hereni mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo katika Kata ya Nala jijini hapo mwishoni mwa wiki, Shekimweri alionya wataalamu hao kuhusu malalamiko ya kuomba rushwa kutoka kwa wafugaji.

"Naomba mkafanye zoezi hili kwa uaminifu nahitaji kusikia idadi ya mifugo iliyopangwa kuvishwa hereni katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma inafikiwa yote," alisema Shekimweri.

Aidha, aliwataka wataalamu kutumia lugha nzuri kwa wafugaji na kuwatumia viongozi wa kimila ili kufanikisha zoezi hilo.

Mkuu huyo alisema endapo zoezi hilo litafanikiwa kwa kiwango kikubwa migogoro baina ya wafugaji na wahifadhi ya kulalamikia kubambikiziwa kesi ya kuingiza mifugo itakwisha.

"Ni vyema suala hilo mkalikamilishe kwa sababu itasaidia serikali kujua nani kaingiza mifugo kutokana na mifugo itakuwa na hereni, lakini kuwatetea wafugaji endapo hawatafanya kosa hilo ili wahifadhi watadai wamefanya," alisema Shekimweri.

Naye ofisa mifugo wa jiji hilo, Gratian Msigwa, alisema wanatarajia kuvisha hereni mifugo 50,000 na Sh. milioni 33 zitatumika katika zoezi hilo.

Alisema ni lazima mifugo yote ichanjwe na kuongeza kuwa atakayekaidi suala hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Aliwahimiza wafugaji kutoa ushirikiano kwa wataalamu wanapoendesha zoezi hilo bila kikwazo.





## Waandishi watakiwa kuwekeza shughuli za kiuchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAANDISHI wa Habari wa Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kujiimarisha kiuchumi na kufanya kazi zao kwa uhuru bila kuingiliwa na watu wengine.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mlezi wa Jukwaa la kiuchumi la wandishi wa habari wa mkoa huo, Ndele Mwaselela, alipokuwa anawakabidhi fedha kwa ajili ya kuwezeshana kiuchumi na hakutaka kiwango cha mchango wake kitajwe.

Alisema waandishi wa habari wakijiimarisha kiuchumi watakuwa na maisha mazuri na watakuwa na uwezo wa kusomesha watoto wao kwenye shule nzuri kama ilivyo kwa watu wengine.

Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za Patrick Mission ya mkoani Dar es Salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya, alisema uwekezaji sio lazima kuwa na mtaji mkubwa bali kinachotakiwa ni nidhamu ya matumizi ya fedha.

Alisema, alikuwa mwalimu wa kawaida, lakini kwa sasa anamiliki shule mbili za kisasa ambazo zinamwingizia fedha za kutosha na hata waandishi wa Mkoa wa Mbeya wanaweza kufikia hatua hiyo.

"Anzisheni biashara ili muutumie muda wenu wa ziada kusimamia, kinachotakiwa ni kuwekeana nidhamu ya fedha ili wanaokopa warejeshe kwa wakati na wengine wakope," alisema Mwaselela.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na waandishi kwa kuwawezesha kiuchumi na kuwapatia elimu ya uwekezaji lengo lake ni kuona maisha ya waandishi yakibadilika.

Kwa upande wake Katibu wa Jukwaa la kiuchumi la waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MJEF), Emmanuel Lengwa, alisema mpaka sasa wanachama wa jukwaa hilo wameshakopeshwa zaidi ya Sh. milioni 10.

Alisema ipo fomu maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya wanachama wanaoomba mkopo kujaza kwa ajili ya kuomba na wanatakiwa kuweka na wadhamini watatu wakiwamo wanafamilia.

# Shule zitakazoshika mkia kupewa adhabu ya vinyago

**Na Nebart Msowa,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya, imeandaa vinyago maalumu vya kutoa adhabu kwa halmashauri na kata yoyote ya mkoa huo ambayo itaburuza mkia kwenye mitihani ya kitaifa ya shule za msingi na sekondari.

Imeanzisha utaratibu huo ili kuongeza hamasa kwa viongozi wa halmashauri na kata za mkoa huo kuongeza usimamizi wa sekta hiyo na kinyago hicho watakuwa wanakaa nacho kwa mwaka mzima mpaka matokeo yatakapobadilika.

Vinyago hivyo vina rangi mbili ambapo cha halmashauri kina rangi nyeusi na cha kata kina rangi nyeupe ili kuvitofautisha.

Aidha, imeandaa makombe maalumu kwa ajili ya halmashauri tatu zitakazoshika nafasi ya kwanza, ya pili na ya tatu kama motisha kwa viongozi wa maeneo hayo kuongeza kasi ya usimamizi wa sekta hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alivitambulisha vinyago hivyo na makombe juzi wakati wa sherehe za utoaji wa tuzo za elimu kwa walimu, wanafunzi, shule na halmashauri zilizofanya vizuri kwenye mitihani hiyo kwa mwaka jana.

Homera alisema vinyago hivyo vilitakiwa vianze kutolewa mwaka huu, lakini akaahirisha kutokana na maeneo mengi kufanya vizuri kwenye mitihani hiyo na akaahidi kuanza kutolewa mwakani.

"Kwa mwaka huu Halmashauri ya Chunya ndiyo ya mwisho na ilitakiwa ipewe kinyago hiki, lakini tumeahirisha kwa sababu Shule ya Sekondari Kiwanja na Kata ya Mjere iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ndiyo ya mwisho na ilitakiwa iondoke na kinyago lakini tumeahirisha," alisema Homera.

Alitoa zawadi mbalimbali kwa walimu waliofaulisha vizuri masomo yao, baadhi ya zawadi zilizotolewa ni pamoja na vyeti na fedha taslimu.

Akitoa taarifa ya hali ya ufaulu katika mkoa huo, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema tathmini inafanyika kwenye mitihani ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita.

Alisema katika tathmini waliyofanya, Halmashauri ya Jiji la Mbeya ndiyo iliyokuwa kinara ikifuatiwa na Rungwe, Kyela, ikashika nafasi ya tatu na nafasi ya ilishikwa na halmashauri za Busokelo na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambazo zilifungana.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilishika nafasi ya sita na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ndiyo iliyoburuza mkia kwenye tathmini hiyo ya jumla.

"Tumetoa tathmini hii kwa mwaka huu na kutoa zawadi hizi ili kuandaa mazingira ya watu kuongeza bidii kwa mwaka ujao, tunataka yatokee mapinduzi makubwa, walioshika nafasi za mwisho waongeze bidii zaidi," alisema Mwalimu Hinju.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, wilayani Chunya, Masache Kasaka, aliipongeza serikali ya mkoa huo kwa kuendelea kutoa tuzo hizo na motisha kwa maelezo kuwa ni utekelezaji wa mikakati iliyotolewa na wadau wa elimu kwenye kikao maalumu kilichofanyika mwaka uliopita.

Alisema wadau walitoa maoni yao kuhusu namna ya kuongeza ufaulu katika ngazi mbalimbali za elimu na zawadi hizo zimeanza kuleta matokeo mazuri.

Aliwataka wadau mbalimbali wa elimu ndani ya mkoa huo kuendelea kushirikiana ili kufikia malengo ya juu zaidi kwenye elimu huku akiahidi kutoa zawadi ya Sh. 500,000 kwa shule 10 zitakazofanya vizuri mwakani na tano kati yake zitakuwa za msingi na zingine tano za sekondari.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera akiwa ameshika vinyago ambavyo vimeandaliwa kwa ajili ya kutolewa kama adhabu kwa halmashauri na kata ambazo zinashika nafasi za mwisho kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa, vinyago hivyo vilizinduliwa juzi wakati wa utoaji wa tuzo mbalimbali za elimu kwa halmashauri, shule na walimu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sekondari mbili zakabidhiwa mabati, madawati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amekabidhi mabati 400 na madawati 200 kwa shule mbili za sekondari za Jiji la Mbeya, vifaa ambavyo alivipokea kama msaada kutoka Benki ya NMB kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa vifaa hivyo shuleni.

DK. Tulia alikabidhi vifaa hivyo katika shule ya Sekondari ya Itende (Dk. Tulia Sekondari) na Shule ya Sekondari ya Itagano ambazo kila moja ilipatiwa mabati 200 na madawati 100.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo katika Shule ya Sekondari ya Itende, Dk. Tulia alisema, kabla ya kupata msaada huo kutoka Benki ya NMB walitembelea shule hizo na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuona mazingira yalivyo.

Alisema wadau walipoona hali ilivyo, wakaahidi kuchangia vifaa hivyo na benki hiyo ndiyo iliyoamua kutoa vifaa hivyo kwa ajili ya kupunguza matatizo ambayo yamekuwa yakizikabili shule hizo.

Aliwapongeza wananchi wa Kata ya Kalobe, jijini humo kwa kuanza ujenzi wa shule hiyo wakitumia nguvu zao kwa maelezo kuwa nguvu zao ndizo zilisababisha serikali na wadau kuamua kuwaunga mkono.

Alisema baada ya serikali kuona juhudi za wananchi hao iliamua kutoa Sh. milioni 470 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo na kisha benki ya NMB kupeleka mabati hayo 200 kwa ajili ya kuezeka.

"Nawapongeza sana wana itende kwa usimamizi mzuri wa mradi huu, mmejenga madarasa yenye viwango na idadi ambayo inaendana na thamani ya fedha iliyotolewa lakini hata maabara mmejenga za viwango vya juu sana hongereni sana," alisema Dk. Tulia.

Alisema serikali inakusudia kupeleka fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu mingine yakiwamo mabweni ya wasichana na nyumba za walimu.

Aliwataka wananchi wa kata hiyo kuendelea kujenga miundombinu mingine kwenye shule hiyo ili wadau wanapojitokeza kusaidia wawe wanaiona miradi ikiendelea kujengwa. Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa, alisema mbali na serikali kutoa fedha hizo zaidi ya milioni 470 kwa ajili ya mradi huo pia imeahidi kutoa zingine Sh. milioni 130 ili zifikie milioni 600 na kwamba mradi huo utakamilika mapema.

Alisema, pia halmashauri imetoa mchango wake ikiwamo kupeleka wataalamu wa kusimamia mradi pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya ijenzi. Vilevile, alisema walipokea pia fedha kutoka Ofisi ya Mbunge wa jimbo hilo kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwamo shule hizo pamoja na shule mbalimbali za jiji hilo. "Tunakushukuru sana Dk. Tulia kwa kutupambania wananchi wa Jiji la Mbeya, kwa miaka mingi wananchi walikuwa hawaoni matumizi ya fedha za jimbo, lakini kwa miaka ya sasa wanaona, tumejenga bweni katika shule zetu mbili za Iduda na Samora Machel na hata hapa zimekuja kwa hiyo tunakupongeza sana Dk. Tulia," alisema Issa.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Trifonia Kisiga, alisema fedha walizopokea kutoka serikalini wamezitumia kujenga vyumba vinane vya madarasa, maabara moja na chumba cha kompyuta pamoja na ujenzi wa matundu 20 ya vyoo.

Alisema mradi huo bado wanaendelea nao na wanakusudia kuukamilisha karibuni ili wanafunzi wanaofaulu kutoka katika shule za msingi za kata hiyo wasiwe wanasafiri umbali mrefu.



# Rais Mwingi aagiza maeneo ya serikali yapewe hatimiliki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka Wizara ya Ardhi, Nishati na Madini kuanza mpango maalum ya kuhakikisha inatoa hatimiliki katika maeneo yote ya serikali ili kuzuia uvamizi.

Alisema hayo katika hafla ya majumuisho baada ya kukamilisha ziara yake katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuna umuhimu wa maeneo yote ya serikali kupimwa na kupatiwa hatimiliki ikiwa ni hatua ya kuzuia uvamizi, huku akibainisha migogoro ya ardhi inayowahusisha wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama tayari imefanyiwa kazi na ripoti yake imeshakabidhiwa ofisini kwake.

Aliipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuja na ubunifu wa kutengeneza shule za elimu mjumuisho, akibainisha hatua hiyo itatoa fursa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata elimu katika mazingira bora.

Alisema kinachohitajika hivi sasa ni kupata walimu wenye fani hizo na kumpongeza mkandarasi wa kituo hicho kwa kazi nzuri.

Pia, ameridhishwa utekelezaji wa mabaraza ya halmashauri ya mkoa huo kwa utekelezaji wa maagizo yake aliyoyatoa katika ziara iliopita, huku akitoa rai ya kuwataka kuongeza bidii katika makusanyo na kuongeza kiwango cha kuelekeza kwenye maendeleo.

Aliwapongeza makandarasi wa hospitali mbili zilizopo mkoani humo kwa kufanya vizuri katika ujenzi na kuwa azma ya serikali ya kuendelea kuwapa kazi wazawa, hatua hiyo itabakisha fedha kwenye mzunguko nchini.

Aliiagiza Wizara Afya kujipanga kwa kuweka mazingira bora ya hospitali hizo ili kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika pamoja na vifaa tiba kupunguza kiwango cha wagonjwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

Dk. Mwinyi aliupongeza uongozi wa mkoa huo kwa kujenga vituo bora vya wajasiriamali, ikilinganishwa na mikoa mingine, huku akilipongeza Jeshi la Zimamoto kwa weledi wa kazi yao.

Alisema wakati wa kampeni wajasiriamali walipewa ahadi ya kuwekewa mazingira bora ya kufanyia biashara zao, elimu, mitaji pamoja na masoko, kinachohitajika ni wao wenyewe kuchangamkia fursa iliyopo.

Katika hatua nyengine, Dk. Mwinyi aliiagiza Wizara ya Uchumi wa Buluu kutafuta njia za kujenga bandari za uvuvi pamoja na viwanda vya kusindika samaki ili kuwawezesha wavuvi kupata soko la uhakika.

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Hadidi Rashid Hadid, alisema mkoa huo una utulivu mkubwa wa kisiasa na uongozi wa mkoa kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa chama na serikali.



Mwanasheria Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Omar Said Shaabani ambaye ni Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar (kushoto), akimkabidhi funguo makamu mwenyekiti wa chama hicho ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ikiwa ishara ya kulifungua jengo hilo, Tunguu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT-Wazalendo yaahidi uchaguzi wa kidemokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kwamba chama hicho kinafanya kazi kubwa ili Zanzibar iwe na mazingira bora ya uchaguzi wa kidemokrasia na kuwezesha kuzuia matatizo ya uvunjivu wa amani wakati wa uchaguzi yasijirudie.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja, alipozungumza baada ya kufungua ofisi za chama hicho Jimbo la Tunguu Mkoa wa Kati Kichama.

Alisema kwa kuzingatia uzalendo na nia njema ya kujiunga na Serikali ya Umoja wa kitaifa, chama hicho kupitia viongozi wake kimekuwa kikishiriki vyema katika kikosi kazi cha kutoa mapendekezo kuhusu uundwaji wa Katiba Mpya ya Tanzania na kwamba kimewasilisha maoni yake kwa maandishi mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika suala hilo. Alisema suala hilo limekuwa likifanywa kwa kuzingatia uzalendo mkubwa unaofanywa na viongozi wa ngazi tofauti kwa nia ya kuhakikisha taifa linajenga mazingira bora ya uchaguzi wa kidemokrasia na amani ya kweli.

Kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othman alisema viongozi waliomo serikalini wanaendelea kujitahidi kuhakikisha anatimiza wajibu wa majukumu ya waliyopewa kwa kuwa wamekula kiapo cha kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na utiifu mkubwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na viongozi kujenga nchi kwa kuunga mkono jitihada za viongozi mbalimbali katika kuhakikisha wanatimiza vyema wajibu waliopewa wa kuitumikia ipasavyo nchi yao.

Kuhusu kauli za ukosoaji kwa viongozi zinazotolewa na chama hicho, Othman alisema kufanya hivyo ni kutekeleza wajibu wa kuisaidia nchi ili iweze kuwatumikia vyema wananchi kwa uzalendo na taifa kupiga hatua za kimaendeleo kwa kasi zaidi.

Akizungumzia suala la Sensa ya Watu na Makazi, aliwataka wanachama wa chama hicho na wananchi kuhakikisha wote wanashiriki kuhesabiwa kwa kutoa ushirikiano ipasavyo siku itakapowadia.

Alisema sensa ni jambo muhimu litakalowezesha taifa kupata takwimu na taarifa sahihi za aina mbalimbali na kusaidia serikali kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia matokeo ya taarifa zitakazopatikana kwenye sensa.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho, Nassor Ahemed Mazrui, alisema viongozi wataendelee kutekeleza majukumu ya kiserikali waliyopewa kwa uzalendo mkubwa ili kusaidia jitihada za unjenzi wa nchi kupitia Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilipo.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Chama hicho ambaye ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema pamoja na majukumu ya kiserikali waliyopewa, pia viongozi wataendelea na jitihada za kukiimarisha chama hicho kwa ujenzi wa ofisi na kuimarisha wanachama katika majimbo mbalimbali nchini.

# Wanane washikiliwa madai biashara dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU wanane wanashikiliwa na Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya baada ya kutuhumiwa kufanya biashara ya kuuza na kusambaza dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo, Kamishna wa Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Kanali Burhani Nassor Zubeir, alisema watuhumiwa hao walikamatwa na viwango tofauti vya dawa hizo huku wengine wakisambaza katika maeneo ya vijijini ikiwamo ukanda wa utalii wa Kiwengwa na Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kanali Zubeir aliwataja watu wanaoshikiliwa na Tume hiyo kuwa ni Ali Abdalla Ali (32), mkazi wa Kiwengwa ambaye alikamatwa na pipi 36 za dawa aina ya heroine.

Wengine ni Ameir Khamis Bakari (36), mkazi wa Mchangani, Wilaya ya Kati Unguja aliyekamatwa na kete sita za heroine, huku Feruzi Abdalla Makame, akikamatwa na kete 30 akiwa katika harakati za kuzisambaza huko Nungwi.

Wengine wanaoshikiliwa na Tume hiyo ni Ameir Dhamiri, aliyekamatwa na mafurushi 10 ya bangi na Emmanuel Joseph, alikamatwa akiwa na bangi kiwango tofauti.

Pia alimtaja Ali Maseka, aliyekamatwa na bangi kiroba kimoja alichokiingiza kutoka Tanga kupitia bandari ya Bumbwini Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kanali Zubeir alisema watuhumiwa hao watafikishwa mbele ya vyombo vya sheria baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa matukio hayo huku juhudi za kuwasaka watu wengine zikiendelea.

Aliwataka vijana kuacha kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya kwa sababu Tume imejipanga kikamilifu kupambana na kudhibiti biashara hiyo haramu.

Aliitaja mikakati yao ikiwamo kuimarisha doria katika maeneo ya bandari na kuwapo kwa bandari bubu zinazofikia 150 ni miongoni mwa chanzo kikubwa cha kazi ya uingiaji na usambazaji wa dawa za kulevya.

Alisema bado wananchi wanatumia bandari bubu kwa ajili ya kusafirisha dawa za kulevya na kwa upande wa kisiwa cha Pemba kinahusishwa na mikoa jirani ya Tanzania Bara ikiwamo Tanga na Mombasa, Kenya katika uingizaji wa dawa hizo.

"Changamoto kubwa katika kupambana na kudhibiti kasi ya uingiaji wa dawa za kulevya ni kuwapo kwa bandari bubu ambazo hutumiwa na wananchi ikiwamo wavuvi kwa shughuli zao za usafirishaji wa bidhaa mbalimbali huku kisiwa cha Pemba kikiongoza," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa Unguja imebainika maeneo ya ukanda wa fukwe katika mwambao wa bahari unaongoza kwa usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kuwahusisha wageni ikiwamo watalii hasa katika vijiji vya Nungwi, Kiwengwa, Pwani mchangani pamoja na Chwaka Wilaya ya Kati Unguja.

## Wakulima pamba Pwani kupata uhakika wa soko

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

HATIMAYE wakulima wa zao la pamba mkoa wa Pwani wanatarajia kuanza kulima zao hilo kwa wingi baada ya kuwa na uhakika wa soko ambalo awali lilisababisha kupunguza kasi ya kilimo hicho hususani maeneo ya Wilaya ya Bagamoyo.

Hayo yameelezwa na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika (CORECU), Mkoa wa Pwani, Musa Mng'elesa baada ya kutembelea katika kikwanda cha pamba kilichoko kata ya Mandera Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo, ambacho kwa sasa kimepata mwekezaji wa Kampuni ya Upami.

Akizungumza baada ya kukagua kiwanda hicho na kuzungumza na baadhi ya wakulima na viongozi wa Vyama vya Ushirika Mng'elesa, alisema kiwanda hicho ambacho ni mali ya CORECU kilitelekezwa kwa miaka 30 iliyopita.

"Baada ya kuingia kwenye uongozi wangu wa nafasi ya mwenyekiti niliwasiliana na Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba nchini na kumwelezea kuhusu uwapo wa kiwanda hiki na waliletewa mwekezaji kwa ajili ya kuwekeza na kusaidia kufufua zao la pamba katika mkoa wetu tuliomba aanze kukikarabati na tayari amefanya hivyo," alisema.

Mng'elesa alisema hatua inayofuata sasa ni kuanza kuwahamasisha wakulima wa mkoa huo kulima pamba kutokana na uhakika wa soko kwani inakubali maeneo yote.

"Natambua vijana wana uhitaji wa ajira na katika kiwanda hiki sio wote watapata ajira, lakini ajira itatokana na kulima na kuleta malighafi katika kiwanda hicho ili kiendelee kufanya kazi," alisema.

Aliiomba Halmashauri ya Chalinze kuwekeza kwenye kilimo kama ilivyo Mikoa ya Kusini katika kukuza mapato kwa kuhamasisha vijana kulima pamba huku wakiwawezesha pembejeo na kuachana na dhana ya kuamini mapato yataendelea kupatikana kwenye kokoto pekee.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Pamba Tanzania, Hussein Kubil, alisema kufufuliwa kiwanda hicho kitarejesha kilimo cha pamba na kuondoa kikwazo cha soko ambacho kilikuwapo awali na kuwafanya wasitishe kulima zao hilo. Alitoa wito kwa wakulima kuanza kulima pamba kilimo ambacho kitawainua kiuchumi na kiwanda hicho kiendelee kufanya kazi bila kusimama ni lazima kiwe na malighafi ya kutosha.

Mwenyekiti wa Chama Cha Ushirika (AMCOS) cha Miono, Iteri Mtewele, alisema uwapo wa mwekezaji katika kiwanda hicho ni hamasa tosha itakayowafanya wakulima kuanza kulima pamba.

"Tunamshukuru mwekezaji huyu kwa ujio wake kwa kuwa mfumo aliokuja nao unashawishi kuwafanya watu warudi kwenye kilimo cha pamba kwa kutoa pembejeo, vifungashio na kuwafuata wakulima moja kwa moja kwenda kununua pamba yao, hii ni hamasa tosha," alisema.

Kodila Mpili na Ally Mhina walisema kufunguliwa kwa kiwanda hicho kitawezesha vijana wao kupata ajira, pia kuanza kulima zao hilo ambalo uzalishaji wake ulisimama kwa kukosa uhakika wa soko.

# Mgodi wabanwa kulipa tozo ya ushuru huduma

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MGODI wa madini ya almasi Williamson Diamond, ulioko wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, umebanwa na halmashauri ya wilaya hiyo kuanza kulipa tozo ya ushuru wa huduma kwa kiwango kinachotakiwa kwa uwiano sawa na uzalishaji wa madini.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson, alibainisha hayo wiki iliyopita kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, wakati akiwasilisha mpango wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo kupitia fedha ambazo zinatolewa na mgodi huo.

Alisema Mgodi wa Almasi Mwadui una umri wa miaka 80 ukichimba madini, lakini halmashauri na wananchi hawanufaiki nao ipasavyo, na kuamua kukaa kikao na uongozi wa mgodi huo na kufikia muafaka kuanza kulipa tozo ya ushuru wa huduma kwa kiwango sahihi.

"Mgodi wa Almasi Mwadui awali ulikuwa ukilipa kiwango kidogo sana cha fedha tozo ya ushuru wa huduma Sh. milioni 150 tofauti na uzalishaji wa madini, baada ya kuwabana wamekubali watakuwa wakilipa asilimia 0.7 wastani wa Sh. bilioni 1.2," alisema Johson.

Alisema, fedha hizo zimeshaingia kwenye akaunti ya halmashauri katika mwaka wa fedha (2022-2023) ulioanza Julai, mwaka huu, ambazo zitatekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kishapu Wiliam Jijimiya, alisema haikuwa kazi ndogo kufikia maafikiano na uongozi huo wa mgodi kulipa kiwango hicho cha fedha na kubainisha kuwa wataendelea kusimamia rasilimali zote zilizopo wilayani humo ili zinufaishe wananchi. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alipongeza madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo kwa kufanya kazi kama timu moja, jambo ambalo limewezesha kufikia mafanikio makubwa ya kupata fedha nyingi kwenye mgodi huo ambazo zitachochea kasi ya maendeleo.

Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo, aliwaomba madiwani wazisimamie fedha hizo vizuri katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili ilete tija kwa jamii na kuonyesha mafanikio ambayo yamepatikana kupitia mgodi huo.




Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti (kushoto walioketi), akiwa pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano kutoka Benki ya Exim, Stanley Kafu (katikati), Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa benki hiyo, Andrew Lyimo (kulia walioketi) na Mkuu wa Matawi ya benki hiyo, Agnes Kaganda (kulia), wakiwa wameketi katika moja ya madawati 100 yaliyotolewa na Benki ya Exim Tanzania kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara. Wengine ni maofisa wa mkoa huo, wafanyakazi wa benki hiyo na wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyejifungua pacha watatu atelekezwa na mume

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kijiji cha Ishila, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, Shija Majaliwa, anadaiwa kumtelekeza mkewe, Magreth Sengeka (30) baada ya kujifungua pacha watatu.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, Magreth Sengeka alisema, alitelekezwa na mume wake Shija Majaliwa Desemba 17, mwaka 2021 hospitalini baada ya kujifungua pacha hao.

Alisema, baada ya kujifungua Shija alifika hospitalini kuwaangalia watoto wake na kuahidi kwenda kuleta fedha za matumizi, lakini mpaka sasa simu yake haipatikani na kusababisha aishi maisha ya shida ya kuomba omba kijijini na kusaidiwa na wanakijiji.

"Mpaka sasa simu yake ya mkononi haipatikani, kwa wazazi wake ni Nzega mkoani Tabora pia hayupo, nimejaribu kufuatilia hakuna msaada wowote niliopata na mpaka leo hii nimejitokeza kwenye mkutano huu ili nipate msaada wa kuwalea watoto wangu," alisema Sengeka.

Alisema maisha anayoishi kwa sasa ni duni, hana makazi ya kudumu na inamuia vigumu kuwalea watoto wake kutokana na kukosa muda wa kwenda kufanya kazi za kumpatia kipato na kujimu maisha na watoto wake.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji Kabogo, Mguzu alisema wanaendelea kuwasiliana na wazazi wa Shija waliopo mkoani Tabora ili kumsaidia katika malezi ya watoto hao ambao kwa sasa wanahitaji uangalizi hususani suala la lishe, malazi na mavazi.

Naye Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga (CCM), Dk. Christina Mzava, alilaani kitendo cha Shija kumtoroka mke wake baada ya kujifungua pacha watatu kwa kusema kuwa wanaume wanapaswa kutokimbia majukumu na badala yake watunze wake zao.

Alisema, watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu, wabunge watahakikisha wanamsaidia ili watoto waweze kukua vyema na kudai kitendo kilichofanywa na Shija ni cha ukatili wa kijinsia na kinapaswa kulaaniwa na kukemewa ili visiendelee kujitokeza katika jamii.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alimsihi Shija popote alipo kujisalimisha ili atunze familia yake kutokana na kitendo alichokifanya kuwa sio cha kiungwana na hakikubaliki katika jamii.

Alisema, yeye na Dk. Mzava wamemchangia Sh. 300,000 kwa ajili ya mahitaji na kuagiza hospitalini anapokwenda kliniki na kupatiwa matibabu asibughusiwe na kwamba kitendo hiki hakipaswi kuvumiliwa katika jamii na kila mmoja atakiwa kupinga vikali tabia hiyo.

HABARI KIMATAIFA

# Iran yafichua mipango ya mashambulizi Israel

**Iran, TEHRAN**

WIZARA ya Ujasusi ya Iran, imetangaza kuwa imewakamata mashushushu wenye mafungamano na shirika la ujasusi la Israel la (Mosad), walioingia nchini humo kwa lengo la kuyashambulia maeneo muhimu ya Jamhuri hiyo ya Kiislamu.

Shirika la habari la Iran, (IRNA) limeripoti likinukuu taarifa ya wizara hiyo kwamba washukiwa hao waliingia nchini humo kutokea kaskazini mwa Iraq lakini walikamatwa kabla ya kutekeleza mpango wao.

Taarifa hiyo haikueleza idadi ya watu waliokamatwa au kutoa utambulisho wa utaifa wao, lakini imewataja kuwa wanachama wanaofanya kazi na kundi la kigaidi linaloshirikiana na shirika la Mosad. Iran hata hivyo haikuainisha maeneo yaliyokuwa yanalengwa kuhujumiwa katika mpango unaodhaniwa kupangwa na washukiwa hao.

Kwa miaka kadhaa nchi hizo zimekuwa zikituhumiana kufanyiana hujuma ikiwamo madai ya Iran kuwa Israel huvishambulia kwa siri vituo vyake vya nyuklia na kuwaua wataalamu wake muhimu ikiwamo wanasayansi. **DW**

# Ugiriki yaendelea kupambana na moto

**ATHENS, Ugiriki**

VIKOSI vya wazima moto nchini Ugiriki vimepambana kuudhibiti moto mkubwa unaoendelea kuwaka kwenye maeneo manne ya nchi hiyo.

Maeneo yaliyoathirika ni pamoja na kisiwa kimoja cha starehe ambako zaidi ya watu 450 wamelazimika kuhamishwa.

Moto ulizuka siku ya juzi asubuhi kwenye kisiwa cha mapumziko cha Lesbos na kupelekea mamlaka kuitisha msaada wa kuwahamisha wageni kwenye hoteli ya Vatera iliyo upande wa kusini.

Zaidi ya wazima moto 300 wakitumia magari, ndege na helikopta walikuwa wanakabiliana pia na moto mwingine unaowaka kwa siku ya tatu mfululizo katika msitu wa taifa wa Dadia unaofahamika kuwa makazi ya idadi kubwa ya viumbe adimu hususani ndege jamii ya Tai.

Maeneo mengine mawili yanayoteketea ni mkoa wa Macedonia Magharibi na kusini mwa mkoa wa Peloponnese.

Ugiriki ambayo hukumbwa na majanga ya moto karibu kila msimu wa kiangazi, ilipatiwa dola milioni 72 kutoka Umoja wa Ulaya mwaka huu kusaidia kuzuia na kupambana na moto. **DW**

# Ukraine yaishutumu Russia shambulio Bandari Odesa

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ameishutumu Russia kwa kufanya kitendo cha kinyama baada ya shambulio la kombora kwenye Bandari ya Odesa.

Shambulio hilo lilifanyika saa chache baada ya kufikiana mkataba wa kihistoria wa kuanza tena mauzo ya nafaka kutoka nchini Ukraine uliotiwa saini saa chache.

Russia bado haijatoa kauli yoyote kuhusu shambulio hilo, lakini Ukraine ilisema maandalizi bado yanaendelea ili kuanza tena mauzo ya nafaka licha ya ukiukwaji huo.

Hata hivyo, Rais Zelensky jana alisema inaonyesha jinsi Russia haiwezi kuaminika katika kuutekeleza mpango huo.

Aliapa kufanya kila liwezekanalo kupata mifumo ya ulinzi wa anga inayoweza kuangusha makombora kama hayo katika siku zijazo.

Ukraine ni muuzaji mkubwa wa nafaka nje, lakini kwa sababu ya vita, takriban tani 20 za nafaka zimenasa katika bandari zake.

Kutokana na hali hiyo, imesababisha uhaba wa chakula na kupanda kwa bei barani Afrika, ambako kwa kawaida inategemea Ukraine na Russia kwa ngano.

Chini ya makubaliano ya Ijumaa, Russia ilikubali kutolenga bandari katika mashambulizi yake wakati usafirishaji wa nafaka unaendelea.

Lakini saa chache baada ya makubaliano hayo kutiwa saini, makombora mawili ya Kalibr yalipiga bandari ya Odesa, kulingana na kituo cha kamandi cha jeshi la kusini la Ukraine.

Makombora mengine mawili yaliangushwa na mifumo ya ulinzi wa anga, iliongeza.

Shambulizi hilo halikusababisha uharibifu mkubwa kwa bandari, kituo cha jeshi kilisema.

Shambulio hilo limelaaniwa vikali.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, aliishutumu Russia kwa kuzidisha mzozo wa chakula duniani, na kusema shambulio hilo lilitia shaka juu ya uaminifu wa kujitolea kwa Russia katika mapatano hayo.

"Russia lazima ikomeshe uchokozi wake na kutekeleza kikamilifu makubaliano ya nafaka ambayo imekubali," alisema Jumamosi.

Ikulu ya Russia haijatoa maelezo yoyote kwa umma kuhusu shambulio hilo, hata hivyo serikali ya Uturuki, iliyosimamia makubaliano hayo, ilisema maofisa wa Russia wamekana kuhusika.

"Katika mawasiliano yetu na Russia, walituambia kwamba hawakuhusika kabisa na shambulio hilo na kwamba walikuwa wakichunguza suala hilo kwa karibu na kwa undani," Waziri wa Ulinzi Hulusai Akar alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban alisema Ukraine haiwezi kushinda dhidi ya Russia.

Akizungumza katika mkutano wa kimataifa wa wahafidhina, alisema vita vinaweza tu kumalizwa na mazungumzo ya amani kati ya Marekani na Russia.

Mkakati mpya unahitajika, ambao unapaswa kuzingatia mazungumzo ya amani badala ya kujaribu kushinda vita," alisema Orban, ambaye maoni yake kuhusu mzozo huo mara nyingi yanakinzana na ya viongozi wengine wa Umoja wa Ulaya.

Mpango huo wa kusafirisha nafaka ulichukua miezi miwili kufikiwa, unatazamiwa kudumu kwa siku 120 na kituo cha uratibu na ufuatiliaji kitakachoanzishwa mjini Istanbul, chenye wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, Uturuki, Russia na Ukraine.

Makubaliano hayo yanaweza kupitiwa upya ikiwa pande zote mbili zitakubali. **BBC**




Mwendesha pikipiki raia wa Ukraine, akiwa anaangalia wingu la moshi unaotokana na mlipuko wa kombora katika Bandari ya Odesa juzi. **PICHA: DW**

# Viongozi wa upinzani wakamatwa

**ANTANANARIVO, Madagascar**

POLISI wa Madagascar jana waliwakamata kwa muda wanasiasa maarufu wawili wa chama kikuu cha upinzani baada ya kufanyika maandamano yaliyolenga kulalamika juu ya hali ngumu ya kiuchumi na kupanda kwa gharama ya maisha. Polisi ilisema imewatia nguvuni Rina Randriamasinoro, ambaye ni katibu mkuu wa chama cha upinzani cha TIM pamoja na mratibu wa chama hicho ngazi ya taifa, kufuatia vurumai iliyozuka kati ya waandamanaji na maofisa wa usalama.

Mamia ya waandamanaji wanaoipinga serikali walikusanyika katikati mwa mji mkuu Antananarivo huku wakifuatiliwa kwa karibu na idadi kubwa ya maofisa wa jeshi na polisi.

Kukamatwa kwa viongozi hao kulichochea zaidi maandamano huku waandamanaji wakiahidi kutoondoka eneo hilo hadi viongozi hao wawili watakapoachiwa.

Hata hivyo iliarifiwa kuwa waandamanaji walitawanyika majira ya mchana na viongozi hao wa upinzani waliachiwa huru baadaye jioni.

**DW**

## HABARI MICHEZO

# NI SOKA LA KIBABE NDANI YA DSTV

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka nchini sasa wakae mkao wa kula baada ya SuperSport kutangaza rasmi kuwa kupitia DStv itaonyesha mubashara michuano maarufu ya soka duniani zikiwamo Ligi Kuu ya England, (EPL), Hispania (LaLiga), Italia (Serie A) pamoja na mashindano ya UEFA Pamoja na Kombe la Dunia.

Akizungumza katika uzinduzi wa msimu mpya wa soka unaofahamika kama Msimu wa Soka la Kibabe, Mkuu wa Masoko wa DStv Tanzania, Ronald Shelukindo, amesema kuwa msimu huu ni moto wa kuotea mbali na Watanzania hawataachwa nyuma kwani nao watakuwa sehemu ya soka la dunia kwa kushuhudia michuano hiyo mubashara ndani ya DStv.

"Kwa hakika huu ni msimu wa soka la kibabe. Na tunamaanisha hivyo kwani sisi DStv tutaonyesha michuano hiyo live na kutufanya na sisi Watanzania tuwe sehemu ya soka la ulimwengu," alisema Shelukindo na kuongeza kuwa kitimtim kitaanza Julai 30 kwenye ngao ya hisani ya nchini England, na mtifuano utaendelea Agosti 5 vumbi la ligi kuu litakapoanza kutimka.

Amesema ili kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanashuhudia na kufurahia michuano hiyo, timu maalum ya watangazaji na wachambuzi wa michezo kwa lugha ya Kiswahili watatangaza na kuchambua michuano hiyo ambapo miongoni mwao ni Abuubakar Liongo, Ibrahim Masoud, George Ambangile, Geoff Lea, Oscar Oscar, Maulidi Kitenge, Ahmed Abdallah na Jemedari Said.

Kama hiyo haitoshi, DStv Tanzania imetoa ofa kabambe kwa wale ambao bado hawana visimbuzi vya DStv ambapo kwa sasa watapata kwa ofa maalum ya Shilingi 69,000 tu ikihusisha seti ya vifaa vya DStv Pamoja na kifurushi cha DStv Shangwe mwezi mmoja.

Amewataka Watanzania kuchangamkia ofa hii ili wasipitwe na burudani ya soka kwani DStv inahakikisha kuwa kila mteja anafurahia burudani hii ya soka.

"Shughuli kubwa msimu huu inatarajiwa ndani ya Ligi Kuu England, huku shauku ikiwa vuta nikuvute kati ya Manchester City na Liverpool ambao wamekamiana na kila mmoja anataka kutwaa kombe msimu huu. Lakini wataalamu wa soka pia wanamwangalia kwa karibu Chelsea na mchawi mwingine Tottenham Hotspur ambao wanaonekana wa moto msimu huu. Lakini je, wakulungwa wa Manchester United chini ya Erik ten Hag watakubali kuachwa nje ya ngoma ya watu wazima? Majibu yote yatapatikana SuperSport ndani ya DStv pekee!"

Huko La Liga nako si haba, muziki wa huko si wa kitoto kwani wakongwe Real Madrid watataka kuendeleza ubabe wao, lakini kuna kigingi cha Diego Simeone na Atletico Madrid ambao nao safari hii wamenoga kwelikweli! Kasheshe haiishii hapo, kwani kuna jabali liitwalo Barcelona chini ya mtaalamu Xavi, hawa nao watahakikisha LaLiga inakuwa ya moto kweli kweli.

Serie A nako ni afe kipa, afe beki! AC Milan bado wanakula urojo wa ushindi wa msimu uliopita, je, wako tayari kunyang'anywa tonge mdomoni? Lakini tonge hilo hilo linatolewa macho na wakulungwa wengine kama Inter Milan ambao ni moja ya timu bora nchini humo bila kuwasahau wazee wazima kina Juventus, Napoli na Roma.

Kwa hakika msimu huu ni burudani ya bandika bandua ndani ya DStv kwani UEFA Champions League, UEFA Europa League na UEFA Europa Conference League nazo zitapeperushwa mubashara ndani ya DStv.

Utamu juu ya utamu utakolea mnamo Novemba na Desemba 2022 ambapo DStv itakuletea mubashara michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika nchini Qatar.

Kwa maandalizi yaliyofanyika Qatar, kwa hakika michuano ya mwaka huu itakuwa ya aina yake. Na DStv nao wamewathamini Watanzania na kuandaa timu mahsusi ya watangazaji na wachambuzi wa soka kwa lugha adhimu ya Kiswahili.




Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso na Mkuu wa Mosoko, Ronald Shelukindo wakiongozwa na msanii maarufu wa Bongo Muvi, Ben Kinyaiya kukagua timu yake muda mfupi kabla ya mechi kati ya timu hiyo na maveterani wa soka iliyofanyika mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. Mechi hiyo ilikuwa na sehemu ya maadhimisho ya ufunguzi wa msimu mpya wa soka ndani ya DStv utakaoanza mwishoni mwa mwezi huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Chirwa, Nyosso watua Ihefu*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ihefu imefanikiwa kuwasajili wachezaji wanne, wakiwamo wachezaji wa zamani wa Simba na Yanga, Obrey Chirwa na Juma Nyosso kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao ambacho kitacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza baada ya kupanda.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo Zagalo Chalamila amesema zoezi la usajili bado linaendelea na watakuwa wakiwatangaza wachezaji wao wapya kila watakuwa wanakamilisha taratibu zote zinazotakiwa.

"Usajili unaendelea, siyo kama tumemaliza, wengine kuna masuala hatujamalisha kwa sababu usajili ni mchakato.

Tunajitahidi kusajili vizuri ili tupate kikosi ambacho kitakuwa na ushindani, hatutaki kurudia makosa tena tuliyoyafanya mwanzo, tunataka kusajili kikosi ambacho ni bora kwa sababu tunaamini msimu ujao ligi itakuwa ngumu zaidi," alisema katibu huyo ambaye timu yake ilishuka daraja msimu wa 2020/21 na kupambana kwa msimu mmoja Ligi ya Championship kabla ya kurejea tena.

Wachezaji wengine waliosajili na klabu hiyo ni Mwaita Gereza kutoka Kagera Sugar na Jaffar Kibaya kutoka Mtibwa Sugar.

Chirwa raia wa Zambia ambaye msimu uliopita aliichezea Namungo FC, akiwahi kuichezea klabu ya Yanga, huku Nyosso aliyesajiliwa kutoka Geita Gold, yeye amewahi kuichezea Simba miaka kadhaa nyuma.

Kuhusu wachezaji wa zamani alisema hawatowaacha, ila kwa wale ambao mkataba wao utakuwa umekwisha watawapa mkono wa kwaheri ili kupata nafasi ya kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa na uzoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Pawasa alia kunyimwa penalti Malawi

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawasa amesema mwamuzi aliyechezesha mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika dhidi ya Malawi hakuwatendea haki, hali iliyosababisha kuambulia kipigo cha mabao 3-2.

Akizungumza baada ya kuwasili hapa nchini kutoka Malawi walikocheza mchezo huo, Pawasa alisema walipata penati mbili, lakini mwamuzi huyo aliwanyima.

"Kwenye mchezo wetu huo tulipata penati mbili, lakini mwamuzi hakututendea haki aliamua kutunyima na sasa tunajipanga kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao tutaucheza Agosti 7, mwaka huu, Dar es Salaam.

Alisema licha ya kupoteza mchezo huo ugenini bado hajakata tamaa na badala yake wanajipanga kwa mchezo wao ujao.

"Wapinzani wetu waliweza kutumia makosa tuliyoyafanya na wakapata nafasi ya kutufunga, lakini hatujakata tamaa," alisema Pawasa.

Alisema tayari amewasoma wapinzani wao hao na kujua sehemu za kuwabana pindi watakapokuja kukutana nao hapa nyumbani.

Michuano hiyo itafanyika Oktoba mwaka huu nchini Msumbiji.

# Yazidu, Kimaro kutwangana

**Na Adam Fungamwango**

MABONDIA wa kike Leila Yazidu na Matha Kimaro wanatarajia kupanda ulingoni na kuzitwanga Agosti nane kwenye Uwanja wa Roma, Makambako mkoani Njombe likiwa ni pambano la raundi nane.

Mratibu wa pambano hilo, Ally Mshindo amesema pambano hilo limepelekwa mkoani Njombe kutokana na maombi ya mashabiki wa ndondi, huku kukiwa na mapambano sita ya utangulizi.

"Mapambano yataanza saa nane mchana na yatawashirikisha pia mabondia wa kike na kiume, huku mabinti wawili na baba yao Said Yazidu watakuwa wanapambana siku hiyo," alisema mratibu huyo.

Alisema ukiondoa pambano kuu, mapambano mengine ya mabondia wa kike watacheza kwa raundi nne, huku ya wanaume wakiwa ni raundi sita.

Aliyataja pambano la utangulizi kwa upande wa wanawake kuwa ni Debora Mwenda atakayepambana na Halima Bandola, huku Hadija Leonard akitwangana na Halima Yazidu.

Mapambano ya wanaume ni West Loyd atakayepambana dhidi ya George Dimoso, Laston Kabuje apanda ulingoni dhidi ya Ajibu Salum, na Amos Kaduma yeye atatwangana na Adam Boika.

## ZISIKUPITE

### RONALDO ANUKIA MADRID

KLABU ya Atletico Madrid imezidisha harakati zao za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, kwa kumweka mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31, kwenye uhamisho huo. (***Times***)

### RONALDO KWA MKOPO

MANCHESTER United itamruhusu Cristiano Ronaldo kuondoka kwa mkopo msimu huu mradi tu awezeshe chaguo la mwaka mmoja kuongeza mkataba wake ili aweze kurejea Old Trafford kwa msimu unaofuata. (***Mirror***)

### KOUNDE NA BARCA

BARCELONA wanatumaini kushinda dau la Chelsea la euro milioni 65 ili kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23. (Sport).

### KIMPEMBE ATAKIWA

CHELSEA itamgeukia mlinzi wa Paris St-Germain na Ufaransa, Presnel Kimpembe mwenye umri wa miaka 26, ikiwa Barcelona itafanikiwa kumsajili Jules Kounde. (***Express***)

### KANE AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imefanya mawasiliano na wawakilishi wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, ambaye hajakataa kuhamia kwa mabingwa hao wa Ujerumani msimu ujao. (***Bild***)

### NEYMAR APUUZA

WINGA wa Brazil, Neymar amepuuza ripoti za yeye kuhama Paris St-Germain msimu huu, huku Chelsea na Manchester City zikihusishwa na mchezaji huyo mwenye miaka 30. (***Mail***)

### DUMFRIES ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili beki wa kulia wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26. (***Calciomercato***)

### LUKAKU KUKAA ZAIDI

CHELSEA wamefikia makubaliano ya kuruhusu Inter Milan kumbakisha mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29 kwa mwaka mmoja zaidi baada ya msimu wake wa awali wa kucheza kwa mkopo wa muda mrefu katika klabu ya Serie A kukamilika. (Mail)

### KLOPP KUTOSAJILI

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amekataa kusajili wachezaji wengine isipokuwa watakapokumbwa na majeraha au kumuuza mchezaji wao yeyote aliyepo. (***Sky Sports***)

### CUCURELLA MAMBO BADO

KLABU ya Brighton imekataa kupunguza bei yao ya pauni milioni 50 na zaidi ya kutaka kumnunua beki wa kushoto wa Hispania, Marc Cucurella baada ya kukataa dau "la kuchekesha" la pauni milioni 30 kutoka Manchester City. (***Athletic***)

### WERNER KUONDOKA

TIMO Werner huenda akaondoka Chelsea msimu huu wa joto kwa sababu mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26 anataka muda zaidi wa kucheza ili apate nafasi kwenye kikosi cha Ujerumani cha Kombe la Dunia. (***Sky Sports***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD AMPA KARIM BENZEMA BALLON D'OR

## Asema ndiye mchezaji anayestahili kutwaa tuzo hiyo mwaka huu na...

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amemuunga mkono mchezaji mwenzake wa Real Madrid, Karim Benzema kwamba, anastahili kushinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu.

**Baada ya msimu mbaya wa 2017/18 ambapo alifunga mabao 12 pekee katika michezo 47, Benzema amejiimarisha tena kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.**

Msimu uliopita aliiwezesha Real Madrid kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kombe la Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ilitajwa kama pambano la Ballon d'Or kati ya Benzema na Sadio Mane (alipokuwa Liverpool) na Mohamed Salah, ingawa tukio hilo liliamuliwa kwa bao la Vinicius Junior.

Lakini akizungumza na ESPN, Hazard alisisitiza kwamba, Mfaransa huyo anastahili kushinda tuzo hiyo sio tu kwa msimu wake bora bali kwa kazi yake nzuri.

"Nadhani (Benzema) anastahili. Unajua, hakuna shaka kuhusu hilo. Lakini nadhani anastahili sio tu kwa msimu huu, lakini kwa kazi yake yote, unajua? Ni kama amekuwa kileleni kwa miaka 15.

"Labda anafunga mabao zaidi, ndiyo maana watu wanataka tu ashinde tuzo hii ya Ballon d'Or, lakini nadhani alistahili hapo awali, kama miaka mitano iliyopita.

"Yeye ni nahodha wetu sasa na pia ni kama, mtu mzuri sana, unajua? Hazungumzi sana uwanjani, anafanya anachotaka. Yeye ni kiongozi wetu. Kwa hivyo tulimsukuma tu kwenda kutwaa Ballon d'Or. "

Tuzo ya Ballon d'Or ya 2022 itatolewa mnamo Oktoba 17.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 295,

MECHI KALI
GAMBA OSAKA
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 14.30
X | 7.06
2 | 1.13

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HATIMA YA NEYMAR PSG HAIJULIKANI




**PARIS,** Ufaransa

KOCHA mpya wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier amekiri kuwa hana uhakika kuhusu mustakabali wa Neymar, licha ya nia ya mshambuliaji huyo kubakia katika klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 30 anaripotiwa kuwa huru kuondoka katika mji mkuu wa Ufaransa, ingawa nyota huyo wa zamani wa Barcelona hataki kuhama.

Neymar amebakiza miaka mitatu kwenye mkataba wake na PSG na alisema Jumamosi kwamba ana furaha kubaki na mabingwa hao wa Ligue 1.

Galtier alifichua kuwa hana uhakika kama Neymar atakuwa sehemu ya kikosi chake msimu wa 2022-23.

"Neymar ana furaha, amekuwa akifanya kazi vizuri tangu mwanzoni mwa maandalizi ya msimu mpya," alisema baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Urawa Red Diamonds.

"Nini kitatokea siku za usoni dirisha la usajili likifungwa, sijui.

"Inatangazwa kwamba anaondoka, na pia inatangazwa kwamba atabaki - sijazungumza na Ney kuhusu hili.

"Lakini haonekani kuwa na wasiwasi kuhusu kile kinachosemwa kuhusu yeye na hali yake katika klabu."

Neymar aliifungia PSG mabao 13 ya Ligue 1 msimu uliopita walipotwaa tena taji lakini hajafunga katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu Machi 2020.



## Klopp kutosajili Liverpool

**LIVERPOOL,** England

HAKUTAKUWA na washambuliaji tena Liverpool katika dirisha hili la usajili, amesema Kocha Jurgen Klopp, isipokuwa kama watapata majeraha au kumuuza mtu.

Wekundu hao tayari wamewaongeza Darwin Nunez, Fabio Carvalho na Calvin Ramsey kwenye kikosi tangu mwisho wa msimu uliopita, na wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumnunua kiungo katika wiki za hivi karibuni.

Jude Bellingham wa Borussia Dortmund na Matheus Nunes wa Sporting CP wameripotiwa kuwindwa, lakini Klopp ameonekana kukataa kuwa na mpango wa kusajili.

Akizungumza na Sky Sports, kocha huyo raia wa Ujerumani alisema alipoulizwa iwapo kutakuwa na usajili zaidi: "Isipokuwa kama tukiwa na majeraha au mauzo ya wachezaji.

"Natumaini, hakutakuwa na (majeruhi) yoyote, kwa hiyo mashabiki wa Liverpool wanaweza kuzingatia mambo mengine."

Mchezaji chipukizi wa zamani wa Fulham, Carvalho amefanya vyema katika mechi za kujiandaa na msimu huu hadi sasa, huku Darwin akifunga mabao manne katika ushindi wa 5-0 dhidi ya RB Leipzig Alhamisi.

## HABARI MICHEZO


,393,790

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/07/22 | 19:00 | Paide Linnameeskond vs Ararat Armenia | 2.82 | 3.22 | 2.47 |
| 02. 28/07/22 | 19:30 | El Gouna vs Ismaily SC | 3.06 | 2.96 | 2.44 |
| 03. 28/07/22 | 19:30 | Farco FC vs Talaea El Gaish | 2.86 | 2.61 | 2.91 |
| 04. 28/07/22 | 19:45 | Maccabi Netanya vs Basaksehir | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 05. 28/07/22 | 19:45 | Elfsborg vs Molde | 2.45 | 3.33 | 2.77 |
| 06. 28/07/22 | 20:00 | Dinamo Batumi vs Lech Poznan | 2.37 | 3.27 | 2.92 |
| 07. 28/07/22 | 20:00 | Olimpija Ljubljana vs Sepsi Osk | 2.52 | 3.19 | 2.78 |
| 08. 28/07/22 | 20:45 | Lechia Gdansk vs Rapid Vienna | 2.54 | 3.30 | 2.69 |
| 09. 28/07/22 | 21:00 | Hamrun Spartans vs Velez Mostar | 2.64 | 3.20 | 2.64 |
| 10. 28/07/22 | 21:00 | FC Vaduz vs Luka Koper | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 11. 28/07/22 | 21:30 | Buducnost vs Breidablik | 2.39 | 3.44 | 2.78 |
| 12. 28/07/22 | 22:00 | Puskas Akademia vs Vitoria Guimaraes | 2.98 | 3.28 | 2.33 |
| 13. 28/07/22 | 22:00 | Coca Cola vs Zamalek | 3.05 | 3.05 | 2.38 |

# MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 25/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1046 | Gamba Osaka vs Paris St Germain | 14.30 | 7.06 | 1.13 |
| 13:00 | 4340 | Bashundhara Kings vs Dhaka Abahani | 2.07 | 3.30 | 3.20 |
| 14:15 | 4850 | Persita Tangerang vs Persik Kediri | 3.23 | 2.84 | 2.28 |
| 15:30 | 3864 | Tromso IL 2 vs Stromsgodset 2 | 3.15 | 4.60 | 1.83 |
| 16:00 | 1998 | CA River Plate (Arg) vs CA Aldosivi Reserve | 1.58 | 3.82 | 4.90 |
| 16:00 | 2800 | Huracan Reserve vs Velez Sarsfield Reserve | 2.95 | 3.64 | 2.06 |
| 16:30 | 2990 | PS Tni vs Persebaya Surabaya | 4.00 | 3.40 | 1.86 |
| 17:00 | 3568 | CA Lanus vs Gimnasia de la Plata Reserve | 2.19 | 3.58 | 2.74 |
| 17:00 | 4998 | CD Godoy Cruz vs CA Union Santa Fe Reserve | 2.71 | 3.15 | 2.42 |
| 17:00 | 5968 | Patronato Reserve vs CA Barracas Central Reserve | 2.30 | 3.19 | 2.85 |
| 18:00 | 5912 | Inter Turku vs Honka | 2.80 | 3.15 | 2.35 |
| 18:15 | 4505 | Septemvri Sofia vs Botev Vratsa | 2.01 | 3.28 | 3.38 |
| 18:30 | 2246 | Kerho 07 vs KPV Kokkola | 2.35 | 3.29 | 2.70 |
| 18:30 | 2945 | Chindia Targoviste vs Hermanstadt | 2.40 | 2.96 | 3.06 |
| 18:30 | 3450 | Pfk Botev Plovdiv II vs PFK Sportist Svoge | 2.15 | 3.06 | 3.25 |
| 19:00 | 1831 | Stjordals vs Blink-Bryne | 2.89 | 3.58 | 2.11 |
| 19:00 | 1832 | Sogndal vs Stabaek | 2.80 | 3.44 | 2.21 |
| 19:00 | 2304 | OKS Odra Opole vs Podbeskidzie Bie | 3.10 | 3.29 | 2.11 |
| 19:00 | 2528 | Sandnes Ulf vs Aasane Fotball | 1.72 | 3.80 | 3.94 |
| 19:00 | 4263 | Kfum Oslo vs Ranheim | 1.85 | 3.72 | 3.43 |
| 19:00 | 5148 | Brann vs Kongsvinger IL | 1.16 | 6.66 | 11.76 |
| 20:00 | 1898 | Wehen vs Borussia Dortmund II | 2.02 | 3.50 | 3.35 |
| 20:00 | 2755 | Norrkoping vs IFK Goteborg | 1.76 | 3.53 | 4.02 |
| 20:00 | 3239 | Stal Mielec vs Radomiak Radom | 2.44 | 3.14 | 2.69 |
| 20:00 | 3395 | Trelleborgs FF vs Skovde Aik | 2.14 | 3.41 | 3.36 |
| 20:00 | 3471 | CS Cerrito vs Danubio FC | 3.67 | 2.99 | 2.03 |
| 20:00 | 3500 | Kjelsaas vs Valerenga IF 2 | 1.24 | 5.90 | 8.07 |
| 20:00 | 3515 | Horsens vs Lyngby | 2.17 | 3.36 | 3.16 |
| 20:00 | 3578 | FC Zenit Saint Petersburg W vs Ryazan Vdv W | 1.11 | 6.46 | 24.47 |
| 20:00 | 3829 | Gjellerasen vs Lillestrom SK 2 | 1.35 | 5.31 | 5.90 |
| 20:00 | 4139 | Eik-Tonsberg vs Sarpsborg Sparta 2 | 1.57 | 4.82 | 3.94 |
| 20:00 | 4761 | KamAZ vs Ska Energiya | 2.75 | 3.04 | 2.45 |
| 20:00 | 5572 | Varbergs Bois vs Hammarby | 6.25 | 4.20 | 1.43 |
| 20:00 | 5615 | Follo vs Fredrikstad FK 2 | 1.60 | 4.60 | 3.86 |
| 20:30 | 2134 | CSKA Sofia vs Cherno More | 2.02 | 3.14 | 3.48 |
| 21:30 | 5374 | 12 de Octubre de Itaugua vs Nacional Asuncion | 3.54 | 3.24 | 1.97 |
| 21:30 | 5640 | UTA Arad vs Petrolul Ploiesti | 1.94 | 3.20 | 3.95 |
| 22:00 | 5026 | CSD Barnechea vs Copiapo | 2.69 | 3.13 | 2.45 |
| 22:15 | 1076 | KR Reykjavik vs Valur | 2.17 | 3.57 | 2.79 |
| 22:15 | 3650 | IA Akranes vs Fram Reykjavik | 2.22 | 3.50 | 2.76 |
| 22:15 | 4754 | Bogota FC vs Deportes Quindio | 2.92 | 2.87 | 2.44 |
| 22:30 | 3974 | San Lorenzo vs Talleres | 2.46 | 2.96 | 2.81 |

## JUMANNE - 26/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1292 | Cerro Largo FC vs River Plate (URU) | 2.44 | 3.05 | 2.76 |
| 00:00 | 4108 | Paysandu PA vs Figueirense | 2.12 | 2.94 | 3.48 |
| 00:40 | 5024 | Deportivo Pereira vs Deportivo Cali | 2.32 | 3.15 | 2.85 |
| 01:00 | 1413 | Union Espanola vs Curico Unido | 2.22 | 3.29 | 2.90 |
| 01:00 | 2206 | Banfield vs Argentinos Juniors | 2.60 | 2.85 | 2.75 |
| 01:00 | 3070 | NewellS Old Boys vs Defensa Justicia | 2.26 | 3.04 | 3.04 |
| 01:00 | 3993 | Criciuma SC vs CSA AL | 2.02 | 2.94 | 3.77 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# KOCHA AZAM FC ATAKA MECHI TATU

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abduhamid Moallin amesema mipango yake ni kucheza mechi tatu za kirafiki wakiwa kambini nchini Misri.

Azam wako katika jiji la El Gouna nchini humo kwa kambi ya siku 20 kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Kuu Bara pamoja na mashindano ya Kombe la Shirikisho (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Moallin alisema watacheza mechi ya kwanza dhidi ya Wadi Degla inayoshiriki Ligi daraja la chini nchini humo.

**Alisema mechi ya pili wa tacheza dhidi ya Suez, na kuhusu mechi yao ya tatu ambayo itakuwa ya mwisho ilikuwa dhidi ya Simba abayo hawatacheza.**

"Kwa bahati mbaya tulikuwa na mpango na Simba, lakini wao watarudi mapema, wakati tunacheza mchezo wa pili wao watakuwa wanarudi Dar es Salaam," alisema.

"Bado tunatafuta mpinzani tutakayecheza nae, nitafurahi nikipata mechi tatu kabla hatujarudi," alisema kocha huyo.

Alisema ana amini kwa namna ambavyo vijana wake wamekuwa wakijituma watakuwa kwenye ubora msimu ujao na kambi itakuwa na manufaa kwao.

Moallin aliongeza wanatambua kwa sasa maandalizi ya msimu mpya ni kuyafanya kuweza kupewa wachezaji mbinu kwa ajili ya kuwa imara.



Nyota wa Azam FC, Ibrahim Ajib (kulia) akiwa na wachezaji wenzake kwenye mazoezi ya programu ya gym kambini katika mji wa El Gouna nchini Misri. **PICHA: AZAM FC**

# *Wasanii watakiwa kujifunza kupiga vyombo*

**Na Sabato Kasika**

MPIGA gita la solo wa siku nyingi ambaye amewahi kuzitumia bendi mbalimbali za dansi nchini, Bonzo Kwembe, amewataka wasanii wa muziki wa kizazi kujifunza kupiga vyombo vya muziki ili kuimarisha vipaji vyao.

Kwembe alisema kuwa kadri miaka inavyokwenda, ndivyo wataalamu wa kupiga vyombo wanavyopungua ikiwamo kufariki dunia, wengine kuwa na umri mkubwa na kushindwa kufanya kazi.

Alisema, katika mazingira hayo, hakuna jitihada zozote zinazofanywa na wasanii hasa wa kizazi kipya za kujifunza kupiga vyombo vya muziki, badala yake wanategemea kupigiwa studio wanapokwenda kurekodi.

"Siyo siri kwamba vipaji vya muziki hasa katika upigaji vyombo vinazidi kupungua nchini kwa kiasi kikubwa, tofauti na miaka ya nyuma ambapo walikuwa wengi, lakini kizazi hiki ni kama hakilioni hilo," alisema Kwembe.

Alisema, muziki kwa maana halisi, ni mpangilio maalumu wa sauti zinazotoka kwenye ala, vyombo vya muziki, zinazopigwa kiufundi, ambapo sauti inayotoka katika vyombo hivyo ndiyo huitwa muziki.

Michezo
Jumatatu Julai 25, 2022
Nipashe




## Hazard ampa Benzema Ballon d'Or

UKURASA 21




Mchezaji mpya wa Yanga, Stephane Aziz Ki (kulia), akiwa na Dennis Nkane kwenye mazoezi ya siku ya kwanza kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa kwenye kambi yao iliyoko Avic Town Kigamboni, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: YANGA**

# Kim ataka zaidi Stars

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa Stars, Kim Poulsen, amesema kwa sasa wanaenda kufanyia kazi madhaifu yao kwa ajili ya kujiimarisha kabla ya mchezo wa marudiano dhidi ya Somalia.

Juzi Stars ilifanikiwa kupata pointi tatu dhidi ya Somalia kwa bao pekee la kiungo wa Azam FC, Abdul Seleman 'Sopu' ukiwa ni mchezo wa kwanza wa kuwania kufuzu michuano ya mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN).

Timu hizo zitarudiana Jumamosi ijayo Uwanja wa Benjamini Mkapa, Stars wakiwa wenyeji kwenye mbio hizo za fainali ya CHAN zitakazofanyika mwakani nchini Algeria.

Akizungumza na gazeti hili, Kim alisema hawakucheza vizuri katika mchezo wao kwanza kwa kushindwa kutengeneza nafasi za kufunga hasa kipindi cha kwanza.

Alisema mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa kwa kutawala mbinu na ufundi hali ambayo hadi wanaenda mapumziko hawakupata bao wala kutengeneza nafasi.

"Kipindi cha pili tumefanikiwa kupata bao pekee, lakini hatukuweza kutengeneza nafasi hili nimeona naenda kufanyia kazi madhaifu yao kwa ajili ya wiki ijayo tunacheza mechi ya marudiano," alisema Kim.

Alisema ataendelea kusisitiza wachezaji wake kuheshimu wapinzani wao kutokana na jinsi ambavyo Somalia walivyocheza, huku mbinu na ufundi ukitawala katika mchezo huo.

Kim alisema wanatakiwa kuwa makini katika mchezo wa marudiano kwa sababu Somalia sio timu ya kuwadharau kuhakikisha wanakuwa makini kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

# MAYELE AANDALIWA MIAKA MIWILI YANGA

## ●●● Mwakilishi aweka wazi, mwenyewe kutua wakati wowote na...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umepanga kuanza haraka mazungumzo ya kuongeza mkataba wa miaka miwili na mshambuliaji wao, Fiston Mayele, kwa lengo la kuendelea kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu ijayo ya mashindano.

Mayele anatarajiwa kuwasili nchini muda wowote kuanzia sasa tayari kwa kujiunga na wenzake kwenye kambi ya Avic Town kule Kigamboni, Dar es Salaam kuendelea na maandalizi ya kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mujibu wa chanzo cha habari, tayari uongozi huo umeshaandaa mkataba na sasa anasubiriwa nyota huyo kwa ajili ya mazungumzo na kuelewana katika maslahi.

**Chanzo hicho kimepasha kwamba, Mayele amebakiza mkataba wa mwaka mmoja ambao unafikia tamati msimu ujao na sasa wanajiweka katika mazingira mazuri kuendelea kubaki nae kwa miaka miwili zaidi.**

"Mayele ana mkataba wa mwaka mmoja, lakini bado tunahitaji huduma yake, sasa tumeanza mazungumzo ya kutaka kumwongezea mkataba mwingine wa miaka miwili," kilisema chanzo hicho.

Hivi karibuni Rais wa Yanga, Hersi Said alisema Mayele bado yuko katika mipango yao na ana mkataba wa mwaka mmoja unaotarajiwa kufikia tamati msimu ujao, lakini wako mbioni kumwongezea mwingine.

Alisema kulingana na mahitaji ya kikosi chao na mipango ya benchi la ufundi la timu hiyo inayoongozwa na Kocha Nesreddine Nabi, mshambuliaji huyo yuko katika mipango na wako katika hatua za kumwongezea mkataba mwingine.

"Suala la kuuza mchezaji kwa sasa halipo, kuhusu Mayele bado yuko Yanga na ataendelea kuwapo, kwa sasa malengo yetu ni kuimarisha timu yetu kufikia malengo ya kutetea mataji yetu yote matatu kwa msimu ujao, lakini kufanya vizuri zaidi michuano ya kimataifa," alisema Rais huyo.

Naye Mwakilishi wa Meneja wa Mayele, Nestory Mutuale, alithibitisha kuwepo mazungumzo hayo na kudai kwamba, kwa sasa Yanga hawana mpango wa kumwachia mchezaji huyo.

"Mayele anatarajia kurejea nchini muda wowote kuanzia sasa na kuhusu kuondoka Yanga ni ngumu kwa sababu hawataki kumwachia na sasa wameanza mazungumzo kwa ajili ya kuongeza mkataba wa miaka miwili," alisema Matuale.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >

***